Kwa Nini?

Habari za jioni, marafiki. Kwa kweli ni majaliwa makubwa kuwa hapa usiku wa leo na, jambo moja, kurudi Arkansas, na, jambo jingine, kuwa kwenye uwanja wa kambi. Ninaamini hii ndiyo mikutano yangu ya kwanza ya kambi ambayo nimehudhuria kwa muda mrefu. Na mimi nilikuwa na mwaliko kuja, na—na kuanza pamoja nanyi. Na mimi nimesikia, kwa kuwa tangu tulipoingia tu, mmekuwa mkiwa na wakati mzuri sana hapa kwenye mkutano huu. Nina shukrani sana kwa hilo.

2 Na, mimi, nikija kule barabarani, dakika chache zilizopita, pamoja na mwanangu, na tulikuwa tunazungumza kuhusu miaka iliyopita wakati nilipokuja huku chini Arkansas kwa mara ya kwanza, ulikuwa ndio wa kwanza wa mikutano yangu. Wakati nilipoanza kwa mara ya kwanza, ilikuwa ni katika Arkansas, katika mikutano aina ya kiinjilisti, hata hivyo. Na tangu wakati huo, nimekuwa mara saba kuzunguka dunia, na sasa nimerudi Arkansas. Ni kama hela chafu, daima huirudisha. Mimi, kila mahali ambapo nimekuwa, nadhani, katika Marekani, nimeuliza, "Watu wowote hapa kutoka Arkansas?" Daima nimekuwa na marafiki kutoka Arkansas, karibu kila mahali. Na daima nimesema: baadhi ya mioyo miaminifu kuliko yote, ninaamini, iliyowahi kudunda, ilikuwa chini ya maskini mashati hayo ya samawati hapa Arkansas. Watu wazuri kweli! Ninawapenda.

3 Na mimi—mimi nina shukrani kwa Mungu kwa ajili ya fursa ya kurudi, usiku wa leo, huku Arkansas, kuwa hapa pamoja nanyi. Na kwa hiyo nafikiri tunazo siku tatu usiku ambazo zimesalia katika mkutano, na kuwa na fursa ya kuja na kuonyesha upendo wangu kwa Yesu Kristo, na kuwa na ushirika na nyinyi watu na kundi letu zuri la ndugu hapa, ambao, wengi wao siwajui. Niliangalia tu kote na kumwona mmoja ninayemjua, Ndugu Jack Moore, ilitokea tu kwamba, na Dada Moore, nilipata kuwatambua wakati huo. Basi kwa kweli tuna furaha kuwa hapa ndani.

4 Sasa, ninajua, siku nzima huna budi kuchoka, mwajua, kuchoka kimwili. Kamwe hatupati ninii ya kutosha... tunachoka tukisifu na kumbariki Mungu, kwa ajili ya wema Wake, jinsi Yeye alivyo wa ajabu. Na, lakini, siku nzima, ndipo basi wakati wa usiku ukija, ndipo hapa ninaingia. Nami kwa namna fulani ni mmoja wa hao wahudumu ambao wamepewa wazo la kunena muda mrefu. Ila sifikiri tutafanya hilo sasa, kwa sababu ya msongamano huu katika mkutano. Mmewasikia wahubiri mashuhuri, hapana shaka, kote katika siku hii na kote katika mkutano. Halafu basi kusimama hapa kwenye jukwaa,

mbona, mbele za hawa wazungumzaji wote hodari, ambao, ninajisikia mdogo kabisa, na kusimama hapa.

5 Mmoja wa wahudumu ndio kwanza nipeane mikono naye, aliniambia hizi ndizo ibada zenu za kwanza kuwa nazo katika maskani hii, ningeliita; sijui hasa tu kile, hekalu hili au chochote lilicho. Na sisi—sisi hakika tuna shukrani tena kwa ajili ya fursa ya kuja katika kanisa jipya, kitu ambacho kimejengwa kwa sifa na heshima kwa Mungu. Jinsi inavyopendeza!

6 Na sisi tumerudishwa tu nyuma, ama si kurudishwa nyuma. . . Ndio kwanza turudi kutoka kwenye. . . kwa ajili ya likizo ya shule kwa watoto. Tunaishi Tucson, Arizona, sasa. Na kumekuwa na joto sana huko nje, bali tunakuta kwamba kidogo kuna joto zaidi hapa nyumbani kuliko kulivyokuwa huko nje, kwa sababu ya unyevu mwingi. Na kwa namna fulani inatuweka chini, baada ya kuzoea hewa ya huko kwa namna fulani.

7 Tuliingia nyumbani na kuwa na ibada ya kwanza Jumapili iliyopita, na sisi tulimwona Bwana Yesu akiendeleza kazi Yake kuu ya upendo na nguvu miongoni mwa watu. Na Injili ile ile ambayo niliwahubiria miaka kumi na mitano iliyopita, hapa Arkansas, ningali ninaamini jambo lile lile. Kamwe msiibadilishe Hiyo. Ni Kristo.

8 Jumapili kulikuwa na jambo lililiotendeka kanisani. Imetokea tu kwamba nimeangalia huku na kumwona yule bwana ambaye mwu—mwujiza ulimfanyikia.

9 Angalia, sisi sote tunapenda ku—kujivunia Bwana Yesu. Tu—tunapenda kufanya hivyo. Nilikuwa na mwanamke wakati mmoja aliyeniambia, alisema hilo ndilo kosa pekee aliloweza kupata kwangu, mimi "hujivuna sana kuhusu Yesu." Nikasema, "Hakika nitaenda Mbinguni kama hayo ndiyo makosa yote niliyo nayo, kujivunia Yesu." Na kwa hiyo mwa—mwanamke huyo hakufikiria Yeye alikuwa ni Mungu. Alijaribu kusema Yeye alikuwa ni mwanadamu tu na mwanafalsafa, ama nabii, au kitu katika utaratibu huo. Lakini mimi nikasema Yeye alikuwa Mungu. Na kwa hiyo sisi . . .

Ndipo yeye akasema, "Ninaweza kukuthibitishia kwamba Yeye hakuwa Mungu."

Nami nikasema, "Loo, siamini kwamba unaweza kufanya hilo."

Akasema, "Loo, ninaweza kuthibitisha Yeye alikuwa tu ni mwanadamu."

10 Nikasema, "Sasa, nitakubali Yeye alikuwa ni mwanadamu, lakini Yeye alikuwa mwanadamu na Mungu pia."

Mwanamke huyo akasema, "Asingeweza kuwa ni Mungu."

Na mimi nikasema, "Loo, Yeye alikuwa ni Mungu, na Yeye ni Mungu."

11 Akasema, “Loo, Yeye asingeweza kuwa.” Kasema, “Nitathibitisha hilo kwa Biblia yako mwenyewe.”

Nikasema, “Vema.”

12 Ndipo yeye akasema, “Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 11, akiwa barabarani kwenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema, ‘Yesu alilia.’”

Nikasema, “Vema, hilo lina uhusiano gani nalo?”

13 Akasema, “Vema, kama Yeye—kama Yeye analia, inathibitisha Yeye si Mungu.”

14 Nikasema, “Mama, hoja yako ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kutokana na kivuli cha kuku aliyekufa njaa.” Nikasema, “Unajua vema kuliko hilo.” Nikasema, “Yeye alikuwa—Yeye alikuwa mwanadamu wakati Yeye alipokuwa anaenda kwenye kaburi la Lazaro, akilia, hiyo ni kweli. Lakini wakati Yeye alipoyanyoosha maskini mabega Yake juu, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku,’ na mtu aliyekuwa amekufa kwa siku nne akasimama kwa miguu yake na kuishi tena, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu, aliyeweza kufanya hilo.” Ningali ninamwamini Yeye kuwa ni huyo.

15 Jumapili, wakati tukizungumza, sisi...Nilikuwa ninawauliza watu wageuke maskanini na kupeana mikono mmoja na mwenzake. Na kulikuwa na ra—rafiki yangu mpendwa, nimejifunza tu kumpenda. Aliingia tu kanisani, yeye na mke wake. Mke wake ni mwuguzi aliyesajiliwa. Na yeye mwenyewe ni Mwingereza. Mke ni Mnorwei. Jinsi hilo lilivyotendeka, sijui. Bali—bali, hata hivyo, wote wawili ni watu wema. Na huyu—huyu ndugu amekuwa na kitu kidogo kasoro, kwa namna fulani moyoni mwake. Na mtu mzuri sana Mkristo, na mtu aliyeelimika, pia, yeye hufanya kazi ya umma kwa ajili ya wahasibu na kadhalika. Na yeye aligeuka, na, alipogeuka, mshtuko wa moyo ukamshika, naye akaanguka chini sakafuni, akafa.

16 Naye mke wake, akiwa ni mwuguzi, alimshika upesi, na kushika mapigo yake ya moyo, “Ameenda.” Ndipo nikaangalia uso wake, mweusi kabisa, macho yake yakageuka nyuma. Si tu kufumba macho yake, bali macho yake yalitokeza nje. Na yeye alikuwa...Nikaja kwenye jukwaa, nikajaribu kunyamazisha kusanyiko, watu wengi walikuwa wanajaribu kumsaidia dada, bila shaka, katika hali hiyo, na mume wake. Mtu fulani aliweka kitu fulani juu ya kichwa chake, ama chini ya kichwa chake, hasa.

17 Nilishika moyo wake, ku...mapigo ya moyo wake mkononi mwake, na hakuna mapigo zaidi ya yalivyo hapo kwenye kipande *hicho* cha mbao. Ndipo basi nikapiga magoti na kuomba, “Bwana Yesu, ninakuomba Wewe, umrudishie Ndugu yetu Way uhai wake.” Na moyo wake ukadunda mara nne au tano, na ukaanza kudunda kawaida tena. Na yeye akarudi

tena, na alikuwa anajaribu kuongea. Asingeweza kuongea, alikuwa . . . Damu husimama, mwajua, moyo ukisita. Na ilikuwa ni muda kabla ya damu yake kuanza kuzunguka sawasawa. Na nikamsikia akiliita jina langu, ndipo basi nikarudi jukwaani.

18 Ndugu Way, sijui kama ungeweza tu kusimama kusudi watu waweze kuona kuwa mtu huyo alikuwa ni nani. Huyo ndiye mwanaume aliyeanguka akafa, Jumapili asubuhi, kutokana na mshtuko wa moyo. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Dada Way, mke wake, mwuguzi aliyekuwa amesimama hapo ili kuchukua mapigo yake ya moyo, kuona. Na kuona kwamba yeye . . . Kwa hiyo mimi . . .

19 Hilo linasikika lisilo la kawaida kabisa, labda, kwa watu ambao wasingeamini mambo haya. Bali nimemwona Bwana Yesu akifufua wafu, mara nyingi. Na hilo si jipya kwetu, kwa hiyo tusingeninii . . . Nafikiri ni sawa kumjivunia Yesu, ila nafikiri inapaswa kuwa ni kweli fulani, kile unachojivunia. Kwa hiyo tumemwona Yeye, nimemwona Yeye, katika miaka kumi na mitano iliyopita, ya visa vingi visivyokosea, akiwafufua wafu.

20 Hasa kimoja huko Meksiko, ambapo mimi na Ndugu Moore tulikuwa tumesimama katika Mji wa Meksiko, maskini mtoto mchanga alifariki asubuhi moja kwenye saa tatu, akiwa na nimonia, katika ofisi ya daktari. Na maskini mwanamke huyo, tusingeweza kumfikisha kwenye . . . Vema, mtu huyo alikuwa amesambaza kadi zote za maombi, na ilibidi tu tuzipe namba vile wangekuja. Hakukuwepo na kadi zaidi za maombi. Basi maskini dada huyu wa Kihispania, yapata, nakisia, umri wa miaka ishirini na mitano, alikuwa na maskini, mtoto aliyefariki; na kulikuwa kunanyesha, na alikuwa naye chini ya blanketi.

21 Na usiku uliotangulia huo, kulikuwa na mwanaume kipofu ambaye alikuwa, loo, labda mwenye umri mkubwa kama baba yangu angekuwa, labda umri wa miaka sabini, kipofu, naye alipokea kuona kwake nilipokuwa nikimwombea. Basi usiku huo, jukwaa lenye upana hasa kama hili lilivyo toka upande mmoja hadi mwingine hapa, lilikuwa tu limejaa malundo, loo, juu kabisa, futi mbili ama tatu, yakiwa tu na shali na kofia, na mavazi makuukuu ambayo walikuwa wameweka pale.

22 Naye maskini mwanamke huyu alikuwa akijaribu kufika pale juu. Naye Billy Paul, mwanangu, alikuja na kusema, "Baba, ninao karibu mabawabu mia tatu pale, na wote mia tatu hawawezi kumshika maskini mwanamke huyo." Alikuwa na mtoto mfu chini ya maskini, blanketi ya samawati.

Nikasema, "Vema," nikamwambia Ndugu Jack Moore, "shuka chini."

23 Mimi na Ndugu Jack Moore tuna mambo mengi yanayofanana. Sitaki kusema tunafanana, kwa sababu yeye ni mtu mwenye sura nzuri sana. Lakini kitu kimoja kuhusu Ndugu Moore, sote wawili hupiga wei nywele zetu kwa njia

sawa. [Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka—Mh.] Tuna mambo mengi yanayofanana. Niliwazia, "Mwanamke huyo kamwe hakunijua," ilibidi waniteremshe chini kwa kamba fulani na kadhalika, kuingia ndani. Kwa hiyo nilimtuma huko chini kumwombea maskini mtoto huyo. Nikawazia, "Vema, hawataninii, kamwe hatajua tofauti."

24 Na kwa hiyo nilianza kuzungumza tena, wakati . . . Ndugu Espinoza, wengi wenu ndugu mnamjua, kutoka Pwani ya Magharibi, alikuwa akifanya ukalimani. Hii ilikuwa huko nje kwenye uwanja wa mafahali ya ng'ombe katika Mji wa Meksiko. Ndipo nikaangalia huko nje kwenye wasikilizaji na nikaona ono la maskini mtoto wa Kimeksiko akiwa ameketi, anatabasamu nami. Kwa hiyo nikasema, "Mlete maskini mama huyo hapa." Kwa hiyo nikaweka mikono juu ya mwili mdogo, baridi, mgumu, uliokufa. Miguu yake ikaanza kurusha mateke, naye akaanza kupiga mayowe, na—naye huyo hapo, hai.

25 Na mimi nikamtuma mkimbiaji, Espinoza alifanya, kupeleleza na daktari, kupata taarifa kabla ya sisi kuiandika. Daktari akaandika hati ya kiapo, kwamba mtoto huyo alifariki asubuhi hiyo katika ofisi yake, yapata saa tatu, na hii ilikuwa yapata saa nne u nusu usiku huo. Na mtoto huyo anaishi leo, akifurahia afya njema, kwa heshima na utukufu wa Mungu.

26 Kwa hiyo tukiona mambo mengi yakitukia, isingetubidi kusema kuhusu Ndugu yetu Way pale, bali ukweli ni ukweli. Na Mungu hafanyi mambo hayo ili tu ku . . . Yeye anataka yajulikane, na watu wajue kwamba Yeye anawapenda. Na kwa neema ya Mungu, Ndugu Way anaketi miongoni mwetu usiku wa leo, anaishi. Tunashukuru kwa hilo.

27 Niliwazia, nikiwa kwenye uwanja wa kambi, nikiingia ndani, sitaki kabisa kuvuruga wakati mzuri. Billy alikuwa akiniambia, alasiri ya leo, kasema, "Wewe huongea kuhusu Pentekoste halisi ya mtindo wa kale," kasema, "wewe ngoja mpaka ufike huko juu!" Kasema, "Wanaimba kana kwamba wamekuwa na ujuzi kwa miaka hamsini."

Nikasema, "Nadhani baadhi yao wamekuwa nao, naam, kwa miaka hamsini."

28 Nami ninapenda kabisa kuingia kwenye mkutano kama huo, ninaamini kila mmoja wetu anapenda, ambapo tunaingia tu moja kwa moja ndani yake.

29 Kama nilivyozoea kusimulia hadithi kuhusu kuvua samaki. Huko juu katika New Hampshire ya kaskazini, nilikuwa nikivua nipate samaki wa mtoni. Basi huko juu kwenye kilele cha mlima, nilikuwa na hema dogo limewekwa huko juu, loo, maskini yale mahema ya-A, hema dogo la watu wawili kutoka kwa serikali. Na nilikuwa nimepata mahali palipokuwa na samaki wengi wa mtoni, palikuwa ni nyuma chini ya kichaka. Na kulikuwa—na kulikuwa na miti mirefu myembamba pale,

na kila wakati nilipojaribu kutia maji tarubali ya mlango wa hema langu, mbona, ingeshikilia kwenye miti mirefu myembamba. Kwa hiyo asubuhi hiyo, niliamka, nikaenda huko juu, mapema, na nikawaza, nitaikata miti hiyo mirefu myembamba. Ningeninii tu. . .Kama nilimwua samaki, basi ningemla, la sivyo ningemwachilia. Kwa hiyo nilikuwa na juma lote, yote niliyoweza kushughulikia, na nilikuwa huko juu peke yangu.

30 Basi nilipokuwa nimeenda asubuhi hiyo, nikiwa njiani nikirudi, maskini dubu jike na maskini watoto wawili walikuwa wameingia ndani ya hema langu. Na wewe unazungumza kuhusu kuharibu vitu, walikuwa wameliharibu kwelikweli. Na walikuwa wamerarua kila kitu. Ndipo ni—nikawazia. . . Niliporudi, nilisikia kelele, na nikaangalia kote kwenye vichaka vidogo nilivyokuwa nikizunguka. Na maskini mama dubu na wote walikuwa tu na wakati mzuri, wakipekua kila kitu.

31 Ndipo akaniona, ndipo akakimbia na akatoa sauti kwa watoto wake. Mmoja wa watoto akaja, na yule mwingine hakuja. Jamaa mdogo, chipukizi, alikuwa tu na urefu *hivi*. Alikuwa ameketi namna *hii*. Nami nikawazia, "Vema, ni nini kinachomvutia sana huyo jamaa mdogo?"

32 Ndipo nikakaribia na kuangalia. Nikamwambia, "Toka hapo! Toka hapo!" Na yeye akaketi tu hapo. Nikawaza. . .Ndipo nikamwangalia maskini mama, kwa sababu, unajua, kucheza na watoto wake, angekuparuza, unajua. Kwa hiyo ni—ni—niliangalia; kulikuwa na mti karibu sana, unajua. Nilikuwa na bastola kuukuu ya kale imewekwa mle ndani ya hema, ilikuwa labda imevunjika wakati huo. Na, hata hivyo, nisingetaka kumpiga risasi maskini mama huyo na kuwaacha mayatima wawili mwituni. Kwa hiyo niliendelea kutazama mti huu, nikizunguka kuona kile jamaa huyo mdogo amevutiwa sana.

33 Na, mnajua, mimi—mimi—mimi ninapenda chapati maji. Sisi, sisi sote ni wa Kusini, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."—Mh.] Magole ndiyo yaliyo huku chini, mwajua. Kwa hiyo, na ninayapenda kwelikweli, nami—nami—ninajua. . . Hakuna Umethodisti mwingi kwangu; ninapenda kweli kumimina sukari ya rojorojo. Ninayabatiza vizuri sana, kuimwaga kote kote juu ya hayo. Kwa hiyo mimi sipendi nyunyizo dogo tu kama unalopata katika sehemu hizi hapa, kitu kidogo. Ninapenda kupata mahali ambapo unaimwagilia kwelikweli, unajua, na kuichanganya vizuri na kuwa nzito.

34 Nilikuwa na ndoo ya nusu galoni iliyojaa ya—ya mtama wa kale. Maskini dubu huyu alikuwa ameondoa kifuniko, na alikuwa anafurahia sukari yangu ya rojorojo kwelikweli. Niliendelea kumwangalia hapo pembeni. Angechukua mguu wake mdogo na kuuingiza ndani ya ndoo hii, mwajua. Na yeye hakujua jinsi ya kutoa sukari hiyo ya rojorojo, kwa hiyo alikuwa

anaingiza tu mguu wake ndani ya sukari yangu ya rojorojo, halafu anauvuta juu na kuramba wakati ukishuka.

35 Nakwambia, hatimaye nilipokaribia na kuvuta usikivu wake, alinitazama. Asingeweza kuniona, alikuwa ni sukari hiyo ya rojorojo kuanzia utosi wa kichwa chake, kote chini. Maskini tumbo lake limejaa sukari ya rojorojo kabisa. Na macho yake, hata asingeweza kufumbua macho yake kunitazama, mwajua, akijaribu.

36 Niliwazia, "Hiyo ni kweli. Hakuna hukumu kwao wanaokula." Inanikumbusha mkutano mzuri wa Pentekoste ya kale, wakati tunapoingiza mikono yetu ndani ya ile balasi ya asali, karibu kina *hicho*, mwajua, cha Asali hiyo ya Kipentekoste.

37 Unajua, jambo la ajabu kuhusu hilo, baada ya kujaza tumbo lake, na ndoo yangu kubaki tupu kwa kuchovya, alienda kwa mama yake na maskini ndugu yake, na mama akamramba.

38 Kwa hiyo, unajua, ninatumai tunapata kiasi fulani juu yetu hapa, hata, tukienda nyumbani, wale ambao hawakuja wataramba kutoka kwetu, ujuzi wetu kidogo, tuwaambie kuhusu mambo makuu ambayo Bwana amefanya hapa chini katika Hot Springs. Bwana awabariki.

39 Basi sasa, ninaamini, waliniambia kwamba hawakuipata kwa wakati mzuri, au kitu kama hicho, kutangaza kugawa kadi za maombi, kuwaombea wagonjwa; namba fulani kwenye kadi, tunawaita na kuwaombea. Na sasa namna hiyo, kwa hiyo imenipa usiku mmoja ili kwa namna fulani kufahamiana. Na kwa hiyo kesho usiku nafikiri wanaenda kusambaza kadi zao za maombi, wakati fulani alasiri. Ndivyo? Naam, tayari ume . . . Saa kumi na mbili? Saa kumi na mbili kesho jioni.

40 Sasa niliwazia, usiku wa leo, tungechukua tu sehemu ndogo ya Maandiko hapa na kusoma Hayo, na kuona kama tungeweza kupata kile ambacho Bwana angependa kutuambia. Na sasa kabla tu hatujafungua Kitabu, hebu tuzungumze na Mwandishi wa Kitabu, tunapoinamisha vichwa vyetu.

41 Kabla hatujaomba, na vichwa vyenu vimeinamishwa; na shughuli zote sasa, na mizaha yote ya siku, na ucheshi kidogo tuliokuwa nao, hebu tuusukume tu kando sasa, kwa kuwa tunamkaribia Mfalme. Je! kuna haja zozote maalum, mngependa kukumbukwa, naomba tu uinue mkono wako, na kusema, "Bwana!" Chini kabisa ndani ya moyo wako, shikilia tu haja yako.

42 Baba yetu wa Mbinguni, tunahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu, Mungu Mwenyezi, kuja katika kusanyiko la Bwana, kushiriki pamoja, tukishuhudia, tukizungumzia mambo makuu ambayo Wewe umefanya, na mahali ambapo tumekuwapo. Na inanikumbusha tu kuhusu Matendo 4, katika Biblia, wakati waliporejea na walikuwa wakizungumzia kile ambacho Bwana

alikuwa ametenda. Ndipo wote wakaomba, na mahali hapo pakatikiswa, walipokuwa wamekusanyika pamoja.

43 Mungu, hatuna hamu kubwa sana, usiku wa leo, kuona jengo likitetemeshwa; ila tungependa Wewe ututikise, Bwana. Tikisa ufahamu wetu. Tikisa utu wetu, msisimko wetu, mioyo yetu ya ufahamu, ili tuweze kutoka hapa usiku wa leo, tukiwa na kusudi zaidi kukutumikia Wewe kuliko wakati wowote, ili tuweze kuhisi Uwepo wa Pentekoste mpya na safi, wa Roho Mtakatifu akijimwaga juu yetu, upya na mara nyingine kama vile huko mwituni na vilimani huko Arkansas, miaka hamsini iliyopita, wakati babu zetu walipokuja kupitia hapa katika farasi na magari, wakihubiri Injili hii. Mpendwa Bwana, tujalie sisi, wabebaji wa Huduma hii kuu stahilifu ambayo Wewe ulituma kupitia hapa, jalia tusionee aibu kitu hiki kikuu; lakini jalia tutembee katika nyayo za wale waliotangulia mbele yetu, Bwana, tukibeba bendera ya Bwana Yesu.

44 Wajalie wengine, ambao hawajaupokea mpango huu mkuu wa wokovu ambao Mungu alituwekea katika Maandiko, iliyotabiriwa kote katika Agano la Kale, na leo hii tunaifurahia, naomba kuwe na kutikiswa kukuu miongoni mwetu, Bwana, na kufanywa upya kwa imani na—na kufanywa upya jitihada.

45 Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya mkutano huu, kwa ajili ya kundi hili la watu ambao wangali wanashikilia, Bwana. Katika saa hii ya majaribu yaliyokuja juu ya nchi, kuwajaribu wale ambao wanakiri kuwa Wakristo, jalia tupatikane, kwenye mwisho, tumestahili kuingia katika furaha za Bwana, ambazo zimetayarishiwa Waliokombolewa, tangu msingi wa ulimwengu. Bariki Neno Lako.

46 Bwana, ukumbuke kila mkono ulioinuliwa. Wewe unajua lengo, Wewe unajua nia, Wewe unajua haja nyuma ya mkono huo. Ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utamjalia kila mmoja. Jalia kila mwanaume ambaye...au mwanamke, mvulana au msichana, aliyeinua mkono, aliyetaka wokovu zaidi, au kutembea karibu zaidi, ama kukujua Wewe kama Mwokozi wao, naomba wasiondoke katika uwanja huu mpaka haja hiyo itakapojibiwa.

47 Kwa wale walio wagonjwa na wahitaji, tunaomba, Mungu, kutakuwa na wimbi kubwa la uponyaji litakalopitia mahali hapa, hata hakutakuwa na mtu mnyonge anayekuja katika uwanja huu atakayeondoka jinsi vile walivyokuja. Wewe uwezaye kumfufua mtu kutoka kwa wafu, na kumleta hapa mbele zetu, inaonyesha kwamba Wewe ni Mungu yeye yule aliyesimama kule karibu na kaburi la Lazaro, ukamwita kutoka miongoni mwa wafu. Baba, wajalie kujua kwamba Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hapa amesimama mmoja miongoni mwetu usiku wa leo, siku chache tu zilizopita, aliyeitwa kurudi kutoka katika nchi mbali zaidi ya kivuli cha ufahamu

wa mwanadamu katika maisha haya. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa hili!

48 Tubariki pamoja sasa tunapojifunza Neno Lako, kwa kuwa kwa kweli Neno Lako ni Kweli. Wewe na Neno Lako ni mmoja. Hawawezi kutenganishwa. Kwa hiyo tunaomba baraka Zako juu yetu, Baba, tunapokungojea Wewe kutunenea usiku wa leo, kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

Sasa, kama mtaweza, ningependa kugeukia Maandiko, na kadhalika.

49 Kwa namna fulani nililala kwenye kitanda na kulala usingizi; muda si muda wajua, Billy akaja na kusema, "Hebu twende."

Kasema, "Unamaanisha ni wakati wa kanisa?" Ilinibidi kutoa lundo dogo la Maandiko niliyokuwa nimetumia hapo kabla, ku—kuzungumza juu yake usiku wa leo.

50 Na nikafikiri labda ingekuwa kwamba wangegawa kadi na kuwaombea wagonjwa, na kadhalika. Nimetambua tangu nilipoingia hapa ndani, watu wawili wamelala kwenye vitanda vya wagonjwa, labda wamekuja kuombewa usiku wa leo.

51 Sasa, ndipo—ndipo Billy akarudi, akasema, "Sikuingia kwa wakati ufaao, baba." Akazungumza juu yake. Kasema, "Tuta—tutaijaribu kesho usiku."

52 Nikasema, "Vema, wewe wapate ndugu, uipate, usambaze kadi."

53 Kwa hiyo sasa ninataka mgeukie pamoja nami, kwenye Ki—Kitabu cha Wafalme wa Pili, na mlango wa kwanza. Halafu basi pia ninataka mgeukie humo kwenye Yeremia, mlango wa 8 na kifungu cha 22. Hebu tusome sehemu tu ya Andiko hili.

> *Ikawa, baada ya kufa kwake Ahabu, Moabu wakawaasi Israeli.*
>
> *Na Ahazia akaanguka katika dirisha la chumba chake orofani, katika Samaria, akaugua; akatuma wajumbe, akawaambia, Enendeni mkaulize kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni, kwamba nitapona ugonjwa huu.*
>
> *Lakini malaika wa* B*WANA* *akamwambia Eliya Mtishbi, Ondoka,* na *uende* na *ukaonane na wale wajumbe wa mfalme wa Samaria, ukawaambie, Je! ni kwa sababu hapana Mungu katika Israeli, hata mnakwenda kuuliza kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni?*
>
> *Basi sasa,* B*WANA* Mungu *asema hivi, Hutashuka katika* kile *kitanda ulichokipanda, bali hakika* wewe *utakufa. Eliya akaondoka.*

54 Na halafu katika Kitabu cha Yeremia, mlango wa 8 na kifungu cha 22.

Je! hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu? mbona basi . . . haijarejea afya ya binti ya watu wangu?

55 Ninataka kuzungumza, kama tungeliita, juu ya somo: *Kwa Nini?* Ni—ni swali, na Mungu anauliza swali hili.

56 Na Mungu ni wa Milele. Tunajua Yeye ni hivyo. Ni wa milele. Yeye hakuwa na mwanzo, au Yeye kamwe hawezi kuwa na mwisho. Umilele kamwe haukuanza, kamwe hauishi, maana ni Milele.

57 Na Mungu hawezi kubadili nia Yake wala njia Yake. Hiyo ndiyo sababu kwamba sisi, kama watu ambao hawatakubali kanuni za imani, kama ni kinyume na Neno, kwa sababu tunaamini kwamba Mungu na Neno Lake ni sawa. Tunaamini kwamba Biblia inasema katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, kwamba, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Hivyo basi Mungu anaposema jambo lolote, Yeye hawezi, kesho au wakati wowote mwingine, kulighairi; wakati Mungu akiwahi kuitwa jukwaani, kufanya uamuzi. Na uamuzi Wake mmoja ni wa Milele. Hauwezi kubadilishwa kamwe.

58 Na Mungu aliitwa kufanya uamuzi kwa jamii ya wanadamu, katika bustani ya Edeni, wakati dhambi ya kwanza ilipotendwa. Je! Yeye angeweza kumkomboa mtoto Wake aliyepotea kumrudisha katika ushirika na Yeye tena? Na Yeye akaweka utaratibu mmoja. Kamwe haujabadilika, kwa njia ya damu. Basi fuata Maandiko, kamwe haujageuka au kubadilika, na kamwe hauwezi, kwa sababu ni uamuzi wa Mungu, kwa Damu. Ingawa, tulijaribu kuubadilisha. Tumejaribu kuuelimisha. Tumejaribu kuundia dhehebu. Tumejaribu kufanya kila kitu kilichoko katika sheria ya mwanadamu, kujaribu kubadilisha Huo, kama Adamu alivyofanya kwa majani ya mkuyu na kadhalika. Lakini ingali inabaki, Damu ndiyo mahali pekee pa ushirika.

59 Hivyo basi, pamoja usiku wa leo, tunaweza kusimama, si kama dhehebu moja, labda wengi wetu pamoja. Lakini hatuwezi kusimama hapa kuwakilisha dhehebu moja, inatubidi kusimama hapa katika ushirika huu chini ya Damu ya Yesu Kristo. Sisi sote tunaweza kuwa ndugu, dada. Mungu hufanya njia kwa mwanadamu, na halafu mwanadamu anakataa kutembea katika njia hiyo, basi Mungu anayo haki kuuliza, "Ni kwa nini hukufanya hivyo?" Na hicho ndicho Yeye alichofanya wakati ule, na hicho ndicho Yeye anachofanya sasa, na hiyo ndiyo sababu Yeye atatenda, kile ambacho Yeye atauliza kwenye Hukumu. Wameuliza, "Kwa nini?"

60 Sasa, somo letu la Maandiko lilianza, punde tu baada ya kifo cha Ahabu, mfalme mbaya, mwaminio wa mpakani, mtu aliyejua jambo lililokuwa sahihi kufanya, na hata hivyo hakuwa

na ujasiri kujitokeza na kufanya lile alilojua lilikuwa sahihi kufanya.

61 Nawazia tu, ikiwa huu—ikiwa ulimwengu huu haukuchafuliwa leo hii na kina Ahabu, ulimwengu huu wa Kikristo tunaoishi ndani yake, umechafuliwa na kina Ahabu, na watu ambao kwa kweli wanajua kwamba ni sahihi kutoa maisha yako na kuwa. . .kwa Mungu, na kujazwa na Roho, na kufuata mafundisho ya Biblia hii, na hata hivyo hawana ujasiri wa kusimama na kufanya hivyo. Inanikumbusha tena juu ya hali nyingine kama hiyo huko Sodoma.

62 Biblia ilisema, "Dhambi za Sodoma, ziliitesa nafsi ya Lutu yenye haki, kila siku." Na jinsi ambavyo nafsi ya mtu huyo ilikuwa yenye haki, na yeye alitazama nje juu ya dhambi za nchi, naye alijua kile ambacho kilikuwa ni kosa, kwamba walikuwa wanafanya kosa, na hata hivyo bila ya ujasiri kutetea imani yake.

63 Si ajabu ulimwengu wote umekuwa Sodoma na Gomora, na jinsi ambavyo kina Lutu leo hii, kote katika taifa na kote ulimwenguni, wakisimama makanisani, ambao wameshawishika kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kwamba nguvu Zake ni halisi tu leo hii kama zilivyowahi kuwa, bila ya ujasiri kusimama mimbarani na kuikataa dhambi, kwa sababu ya kizuizi fulani ambacho kingewafukuza kutoka kwenye ushirika ambao walikuwa wamejiunga nao. Bado inarudi kwenye Damu ya Yesu Kristo, suluhisho la pekee.

"Kwa nini? Kwa nini?"

64 Ahazia alikuwa—alikuwa mwana wa Ahabu, alikuwa amelelewa katika aina ya nyumba ambayo—ambayo ilikuwa nyu—nyumba vuguvugu. Haikuwa kabisa ya Kikristo. Mama yake alikuwa kafiri. Na baba yake alikuwa ameoa nje ya ushirika, akamwoa mwanamke ambaye hakuwa mwaminio.

65 Na hiyo daima hufanya makazi mabaya kwa mtoto yeyote kulelewa ndani yake, kwamba wakati kutokuamini na imani zinapojaribu kuchanganyikana pamoja.

66 Na, sasa, kama baba angalikuwa ni mtu hodari kwelikweli kwa imani yake, mtoto huyo pengine angalikuwa na nafasi bora, lakini ha—hakuwa nayo. Hakuwa nayo. Alijua kwamba kulikuwa na Mungu. Alijua kwamba kulikuwa na Yehova. Ndipo basi yeye. . .miungu wa mama yake, na kadhalika. Alichanganyikiwa kabisa. Halafu baada ya kifo cha baba yake, mvulana huyu katika hali hii, kwa namna fulani amechanganyikiwa, kwa njia moja na nyingine.

67 Na kama hiyo si picha ya nchi leo hii! Mmoja katika familia yuko *hivi*, na mmoja vingine, na mmoja anaelekea *huku* na mwingine anaelekea *kule*. Si ajabu tunaleta upotovu mwingi wa watoto, na namna zingine zote za mambo, chini ya jina la

Ukristo. Ni kwa sababu hakuna umoja. Hakuna wito halisi wa kutoka, na kumtetea Mungu.

68 Sasa tunaona kwamba, jamaa huyu anakuwa mrithi wa enzi ya baba yake. Siku moja, juu katika kilele cha roshani yake mahali fulani, akitembea huku na huku, a—alianguka kupitia di—dirishani. Huenda alilewa kupita kiasi na akaanguka kupitia dirishani, chini labda kwenye orofa ya chini, akagonga dawati ama kitu fulani, na kuvunja mbavu chache au kujeruhiwa. Na ugonjwa hapana shaka ulianzisha maambukizi mahali fulani, ama jeraha, na kumsababisha kuwa na homa. Naye alikuwa mgonjwa sana.

69 Bila shaka, siku hizo, hawakuwa na tiba walizo nazo sasa. Labda madaktari walikuja na kufanya waliyoweza kwa jamaa huyo, ila hawakuwa na utoshelevu. Ndipo alijua kitu chake pekee alichoweza kufanya kingekuwa ni kuenda kwa mamlaka ya juu kuliko kile ambacho madaktari wangeweza kuzalisha katika lugha yao ya tiba. Ndipo akawazia angeenda basi; na akatuma mtu kwa mama yake.

70 Somo la jinsi gani hilo linapaswa kuwa kwa kina mama! Mtoto kwa kawaida atamsikiliza mama yake.

71 Naye alienda kwa wake, akatuma watu kwa Mungu wa mama yake, Baal-zebubu, huko Ekroni, mahali sanamu yake ilikuwepo, sanamu ya ukumbusho wake. Ndipo kasema, "Nendeni mkawatake ushauri makuhani huko, na hebu waitake ushauri sanamu yao ya Baal-zebubu, kama nitapona ugonjwa huu nilio nao, au la."

72 Bali mnajua, mtu huyo, kweli, mngeweza kuwazia? Watu waliodhaniwa kuwa ni watu wacha mungu, wangeacha mtu kama huyo awatawale, ni kwa sababu ya hali ya uvuguvugu. Ilikuwa ndiyo hali ambayo kanisa lilikuwa limeingia ndani yake, iliyomweka mtu kama huyo mamlakani, au kuruhusu hilo. Sidhanii kuwa nyakati zimebadilika sana; zingali zinaonekana kwa sehemu kubwa kuwa vivyo hivyo. Na kumwacha mtu huyu atawale, kuwa na usemi juu ya taifa, ambaye angetafuta ushauri kutoka kwa sanamu fulani ya wazo la kikafiri kuhusu hali yake.

73 Na kisha, unajua, bali nyuma ya hayo yote, haijalishi ni kiasi gani inaonekana kwamba Mungu amegeuza uso Wake kutoka kwa watu, Yeye hufanya hivyo wakati mwingine kuona aina ya msimamo unaochukua. Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa na kurudiwa.

74 Na halafu pana mahali padogo ndani ya mwanaume, au mwanamke, wakati wakizaliwa na Roho wa Mungu, ambapo ni pa Milele.

75 Na utafikia mahali wakati mwingine ambapo kila . . . Kila kitu kilicho cha kibinadamu kukuhusu, katika kuhojiana, ibilisi anaweza kukiondoa kwako kwa mahojiano. Lakini wakati inaposambaratika, ndipo, ikiwa huo Uzima wa Milele haupo

hapo, utaanguka pia, kwa sababu unaweza kujiondoa kwa Mungu kwa kuhojiana.

76 Bali mtu anayedai kuwa Mkristo, hana haki mimbarani, ama hana haki katika ofisi, kiongozi popote, mpaka kwanza avipande hivyo vipandio kuingia mahali ambapo amezaliwa na Roho wa Mungu, akajazwa na Roho Mtakatifu, hivi kwamba hakuna mtu awezaye kuliondolea mbali kutoka kwake kwa maelezo.

77 Mungu, wakati Yeye alipomtuma Musa huko chini Misri, kuwakomboa watu, kwanza Yeye alimpeleka upande wa nyuma ya jangwa, na kuondoa theolojia yote aliyokuwa nayo ndani yake, katika miaka arobaini, ndipo akamtokea. Alijua mengi kuhusu Mungu, katika dakika tano, katika Uwepo wa kichaka kile kilichowaka moto, kuliko aliyojua katika miaka arobaini ya kujifunza aliyopata.

78 Hilo ndilo kanisa linahitaji usiku wa leo, ni tukio jingine la kichaka kinachowaka moto, ambapo watu wenye ulimi mwepesi. . .Ambapo, Maandiko yanasema kwamba, "Roho hizo mbili katika siku za mwisho zitakaribiana sana, ingewadanganya wateule kama yamkini."

79 Mtu anapaswa kwanza kuingia mahali hapo patakatifu pamoja na Mungu; ambapo wanatheolojia wote, madaktari wote wa elimu ya kiungu, hoja zote, wote wasiosadiki kuwa Mungu yuko, hakuna chochote kingine kiwezacho kufafanua hilo na kuliondoa kwake. Alikuwepo pale wakati Mungu alipokuja, na anajua kilichotukia. Huwezi kulihoji na kulitoa kwake; alikuwepo wakati lilipotendeka. Huyo ndiye aina ya mtu tunayehitaji leo hii katika serikali, kanisani, na popote pale, katika nyakati kama hizi. Kwa ajili ya uongozi, tunahitaji mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu.

80 Hilo ndilo kanisa linalohitaji leo hii; si mwanatheolojia, bali mtu aliyejazwa na Roho, aliyezaliwa upya, aliyejawa Roho Mtakatifu. Nakwambia, kama tungekuwa na zaidi ya hilo, kanisa lingeonekana tofauti kidogo kuliko linavyoonekana katika wakati wa sasa. Mambo yangekuwa tofauti kama tungekuwa tu na watu zaidi waliojazwa na Roho wa Mungu, sio kufuata desturi za wazee, na kadhalika.

81 Sasa tunaona kwamba jamaa huyu alituma watu huko juu kupata habari hii kutoka—kutoka kwa—kutoka kwa mungu wa Ekroni, Baal-zebubu.

82 Bali, wakati wote, Mungu alijua kuwa alikuwa anafanya hivyo. Kwa hiyo Yeye alikuwa na nabii huko chini, jina lake Eliya, kwa hiyo Yeye akanena na Eliya na kusema, "Nenda huko juu kwenye barabara fulani, na usimame katika njia hiyo. Wajumbe wanakuja." Unaona, huwezi kuficha chochote kutoka kwa Mungu, unaona, haijalishi kile unachofanya. Sasa, jamaa huyo hakujua kuwa Mungu alikuwa akinena na Eliya huko chini nyikani mahali fulani, katika kibanda kidogo cha matope mahali

fulani, na angeweza kumwambia "Nenda, usimame pembeni mwa barabara kule juu, na uzungumze na jamaa hawa, na uwaambie 'Warudi huko chini kwake, na kumwambia, "BWANA ASEMA HIVI, yeye hatoki kwenye kitanda hicho."'"

83 Tena Yeye akasema, "Mwulize, 'Kwa nini ulifanya hivyo? Ni nini kinachokufanya kufanya hivyo? Ni kwa sababu kwamba hakuna Mungu Israeli? Je! ni kwa sababu Yeye hana nabii? Je! hiyo ndiyo sababu ulifanya hivyo? Mbona, unajua kile kilichotendeka. Unajua Maandiko. Unayo katika ikulu yako mwenyewe. Makuhani wako karibu hapo. Hapana shaka umeyasoma tangu ulipokuwa mvulana. Basi ni kwa nini ulifanya jambo la kijinga kama hilo?'"

84 Nashangaa, usiku wa leo, kama Kristo angekuja jukwaani, ama kote katika taifa leo hii, katika kuleta taifa hili kwenye hukumu, kama swali lilo hilo halingeulizwa. Ni kwa nini hivyo, ndivyo? Ni kwa nini tunafanya mambo haya? Ni kwa nini tunazozana katika serikali, kama inafaa tusome Biblia hadharani, na, kwa nini, kama tunasoma upuuzi huu wote? Je! si babu zetu waliiweka katiba hii katika utaratibu? Je! taifa hili halikuzaliwa juu ya misingi ya Biblia? Si tupo hapa kwa ajili ya uhuru wa kidini, kutenda katika Mungu jinsi tunavyojisikia sawa kutenda, jinsi ambavyo tumeshawishika kwamba ni Kweli?

85 Bali, unaona, tumefanya jambo kama walilofanya wakati ule. Tunaruhusu tu kila kitu, siasa, kutumeza, badala ya kuiheshimu Imani yetu katika Mungu wetu, na watu ambao wamesimamia Kweli. Na sisi tunaacha siasa zetu zikanyage hilo, na kupiga kura katika mambo kama hayo yanayochafua taifa hili, na wakati tunakuja kwenye hukumu. Mungu atainuka jukwaani, siku moja, akiwa na nabii mwenye nguvu, anene katika kizazi hiki na—na kuwaambia watu, ndipo wao wataona kwamba ni Mungu ananena, ila hawatatubu. Itakuwa tu kama ilivyokuwa wakati ule.

86 Akasema, "Je! hakuna Mungu katika Israeli? Je! ni kwa sababu hakuna Mungu?" Sawa na Yeremia alivyosema, "Hivi hakuna zeri katika Gileadi? Hakuna tabibu kule?" Basi, wasingeweza kujibu hilo. Bila shaka, alikuwepo. Vema, Yeye alisema, "Basi, kwa nini, kwa nini ulifanya hivyo? Ni kwa nini haijarejea afya ya binti ya watu wangu?"

87 Sasa tunashangaa hilo, usiku wa leo. Kwa nini? Hivi hakuna Biblia? Hivi hakuna Mungu? Hivi hakuna tofauti? Kama Mungu anaenda kuleta watu Hukumuni, inambidi Yeye kuwa na kitu cha kuwahukumu kwacho. Hapana budi kuwepo na kigezo fulani.

88 Ikiwa Yeye anaenda kuwahukumu kwa kanisa Katoliki; basi wakiwahukumu kwa kanisa la Kirumi, kanisa la Kiyunani limepotea, makanisa mengine ya Katoliki yamepotea. Kama

Yeye aliuhukumu kwa la Kiyunani, la Kirumi limepotea. Kama Yeye aliuhukumu kwa la Kilutheri, la Methodisti limepotea. Kama Yeye aliuhukumu kwa la Methodisti, la Kilutheri limepotea. Hawezi kuuhukumu kwa kanisa; yapo madhehebu mengi sana mbalimbali ya hilo.

89 Lakini Mungu atauhukumu ulimwengu, Yeye alisema, kwa Yesu Kristo. Na Yesu Kristo ni Neno, nalo Neno ni Mungu. Na Yeye atawahukumu kwa Biblia hii, kwa sababu hii ni Neno. Hicho ndicho kipimo cha Mungu. Lazima tufikie kiwango kile Biblia isemacho.

90 Na sisi tunashangaa ni kwa nini tuna mchafuko mwingi, madhehebu mengi sana, tofauti nyingi, kutenga udugu, na—na kila kitu. Ni kwa sababu hakuna Zeri katika Gileadi? Ni kwa sababu hakuna tabibu huko? Sijui kama Mungu angetuuliza hilo swali?

91 Sasa, haikuwa—haikuwa hasa kwamba hawakuwa na Tabibu. Walikuwa naye. Mungu alikuwa ndiye Tabibu. Na haikuwa kwa sababu hakukuwa na Mungu Israeli. Kulikuwa na Mungu. Pia walikuwa na nabii wa kumtaka shauri, kujua kwamba mambo haya ni nini. Lakini yalikuwa ni mapenzi makaidi ya mfalme mwenyewe. Hiyo ni hakika.

92 Na hiyo ndiyo shida katika taifa leo hii. Ni mapenzi makaidi ya watu wenyewe. Si kwa sababu hatuna Mungu yeye yule aliyevuka Bahari ya Shamu, pamoja na watu Wake, ambaye aliwalisha miaka arobaini nyikani. Si kwa sababu hatuna Mungu yule yule tuliyekuwa naye hapo mwanzo. Ni njia kaidi ya watu wenyewe. Hawataki kunyenyekea. Hawataki ku—kuwa na uhusiano wowote na utakatifu na usafi wa kuishi njia ya Biblia ya kuishi. Heri wawe wafuasi wa kanisa na kuweka jina lao kwenye kitabu, na kuishi kama ulimwengu wote ulivyo, kuliko kujinyenyekeza kwa ahadi na Amri za Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo shida leo hii. Hiyo ndiyo sababu mambo yanaenda jinsi yalivyo, watu wanaondokea Neno. Kamwe hutaweza kunyooshwa mpaka turudi kwenye njia sahihi.

93 Walijenga jengo hili, wakaweka kona hiyo *hapa* chini mahali fulani, usingeweza kulifanya jengo lijengwe. Inakubidi kuwekwa kwenye msingi. Nao msingi ni Biblia, mafundisho ya mitume na manabii, na kadhalika, ya Biblia.

94 Njia kaidi ya mfalme mwenyewe. Yeye hakutaka tu ku—kutuma watu huko chini. Halikuwa maarufu sana.

95 Njia halisi ya kweli ya Mungu ya kuishi haijawahi kuwa maarufu. Kamwe haitakuwa maarufu. "Kwa kuwa kuhubiriwa kwa Injili ni upumbavu kwao wanaoangamia." Paulo alisema, "Siionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwani ndiyo nguvu za Mungu ziletazo wokovu kwao wanaoamini."

Sasa tunakuta hapa kwamba mfalme alikuwa mkaidi.

96 Kitu tu kama leo hii, mgonjwa atalala moja kwa moja kwenye. . .Vipi kama mgonjwa alienda kwa daktari na kulala kwenye vipandio vyake, na alikuwa na namna fulani ya ho—homa iliyokuwa inaenda kumwua? Naye daktari akaja mlangoni, na kusema, "Bwana, ninayo dawa humu ndani."

Aseme, "Ah, mimi siingii."

"Ingia ndani, nitakudunga sindano, chanjo."

"Sitaki dawa yako."

97 Na kusema sasa, "Bwana, ni—ninaweza kukusaidia ikiwa tu utaingia ndani."

"Vema, siingii ndani."

98 Na mtu huyo akalala hapo kwenye vipandio vya daktari na akafa; kufa kwenye vipandio vya daktari kwa sababu asingekubali chanjo ya homa ya matumbo ama chochote kile, alichokuwa nacho. Hatakubali chanjo yake, na mtu huyo anakufa moja kwa moja kwenye mlango wa daktari. Sasa, mtu huyo. . .Huwezi kumlaumu daktari, kama yeye ana da—dawa ambayo ita—ambayo itaponya ugonjwa huo, naye daktari yuko radhi kumpa, na imetolewa. Na mtu huyo akaketi, akaja karibu hata kufikia mlangoni pa daktari, na kuketi chini hapo na akafa, huwezi kumlaumu daktari. Huwezi kuilaumu dawa. Ni mtu huyo ndiye anafaa kulaumiwa; akifa kwenye mlango wa daktari, akiwa na ugonjwa ambao kuna dawa ya kutibu, inayoweza kuutibu, ndani. Vema, hiyo tu ni methali.

99 Lakini, mnajua, Mungu anayo dawa ndani ya Ufalme Wake, ambayo itatibu kila ugonjwa wa dhambi ulioko ulimwenguni, nao watu wanakaa moja kwa moja kwenye mlango wa kanisa. Si hivyo tu, bali wanaketi moja kwa moja kwenye kiti cha kanisani, na kufa, na wanapotea na kuenda Kuzimu, kwa sababu wanakataa kukubali dawa ya Daktari. Amina. Hiyo ni kweli. Wanakataa kabisa kuchukua dawa ya Daktari, kwa hiyo wanakufa na homa.

100 Na watu wanakaa kanisani na kusikia Jumbe za Mungu, na kuziamini, na hawatakubali Hiyo. Wasingeweza kusema, "Vema, sasa siamini hiyo ni kweli." Baadhi yao watakuja, waseme na kukubaliana na Hiyo, waseme, "Ninaamini Hiyo ni sahihi," bali hamtafanya hivyo. Unaona, utakufa. Wanakufa katika viti vya kanisani, kwa sababu hawatakubali tiba. Hawatakubali. Unaona, kile ifanyacho, inaondolea mbali u—umaarufu kidogo kutoka kwa watu. Kwa namna fulani inawapiga kidogo.

101 Wanaogopa huko Kuzaliwa upya. Mnajua, uzazi wowote ni mchafuko. Sijali ni nini, kama ni katika kizimba cha nguruwe au hospitali iliyopambwa rangi ya waridi, ni mchafuko, na ndivyo kulivyo Kuzaliwa upya. Kutakufanya utende mambo ambayo hukudhania ungeweza kutenda. Kutakunyoosha. Lakini kabla hujaweza kuwa sawa, inakubidi kupitia mchafuko huo. Hiyo

ni kweli. Amina. Kabla mbegu kuweza kuzaliwa, lazima ife na kuoza. Na hiyo ndiyo shida ya watu leo hii, hawataki kufa na kuoza kwa ulimwengu, ili waweze kuzaliwa upya kwa Roho Mtakatifu. Unaona, hiyo ni kweli. Wanakuogopa huko Kuzaliwa kupya. Wana—wanaogopa.

102 Huwafanya kufanya mambo ambayo hawataki kufanya. Kunaondoa umaarufu kutoka kwao. Kunaondoa ugumu kutoka kwao. Loo, nakwambia, nina furaha kwamba kuna chanjo, usiku wa leo, itakayouondoa kutoka kwako, ndugu, itakayouondoa ulimwengu. Itafanya watu, udugu, washirikiane pamoja bila ya kujali tofauti za kimadhehebu. Ita—itafanya jozi ya ovaroli kukumbatiana na suti rasmi, na kupiga makelele, "Ndugu, nina furaha kukuona!" Amina. Hakika! Bali wewe. . . Wanaogopa chanjo hiyo. Loo, jamani!

103 Ni hatari kukataa dawa ya daktari, mwajua, kama wewe—kama unaenda kwake. Na inaogopa . . . Ukikataa dawa, ni hatari. Huenda ukafa. Lakini hiyo, hiyo, utakufa tu kimwili, kutokana na kutochukua dawa ya daktari. Lakini jinsi ilivyo hatari zaidi kukataa chanjo ya Mungu kutokana na dhambi!

104 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa na kipindi kidogo cha ugonjwa, ndipo mtu fulani akaniambia, kasema, "Vema, Billy," kasema, "hivi uliishikilia dini yako wakati wa ugonjwa wako?" Kasema, "Unajua, wewe unaamini uponyaji wa Kiungu; hivi ulishikilia dini yako?"

105 Nikasema, "La, ilinishikilia. Si wazo la mimi kuishikilia; hiyo hunishikilia."

106 Wakati Damu ya Yesu Kristo ilipomwagwa Kalvari, Mungu alifanya maandalizi. Wakati mwanadamu alipotenda dhambi mara ya kwanza, aliacha mwenyewe shimo kubwa ambalo alivuka, akijiacha mwenyewe bila njia ya kurudi. Mungu, aliye mwingi wa rehema, alikubali kibadala, na hicho kilikuwa ni damu ya mwana-kondoo au fahali, na kibadala hicho kilidumu kwa miaka.

107 Musa alisimama chini ya uvuvio wa Mungu, wakati dhambi hata haikuwa imeondolewa, ilikuwa tu imefunikwa na damu ya mafahali na mbuzi. Na yeye alikuwa na u—utukufu wa Mungu juu yake, mpaka angeweza kunena nzi wakawepo, angeweza kunena vyura wakawepo. Kwa sababu, neno ni wazo lililodhihirishwa, na Mungu alileta mawazo Yake kwa Musa, ndipo Musa akayanena katika maneno. Na wakati Neno liliponena, ulimwengu wote uliumbwa na Neno la Mungu.

108 Kulikuwa na wakati ambapo ningepata, katika shule, kupata wino mweusi kwenye ninii langu—kwenye shati langu. Mama alizoea kuvua shati langu, na kusema, "Nipe hilo, upesi, mpenzi," ndipo yeye angeweka mafuta ya makaa juu yake. Na yote yaliyofanya ni kuutawanya kabisa, ukafanya duara kubwa

la doa, ambapo aliweka mafuta ya makaa kwenye wino. Hayo ndiyo yote aliyojua. Hicho ndicho bora zaidi alichokuwa nacho.

109 Bali ni tofauti leo hii. Wametengeneza bidhaa iitwayo kipausha. Na wewe . . . Ni kemikali ambayo wakati wowote wino unapoanguka kwenye hiyo Kloroksi, au kipausha, chochote kilicho. Ukianguka kwenye hiyo, huwezi kupata weusi huo tena, hata kidogo. Ni nini kinachoufanyikia? Dondosha tone la wino mweusi katika beseni ya kipausha, mbona, huna chochote. Huwezi kupata mvuke wowote.

110 Kama ningalikuwa mwanakemia, ma—maneno haya huenda yasiwe kweli hasa kwa sayansi, bali ningesema, ni kitu gani? "Ni H_2O, maji, kwa kitu kimoja. Basi kuna kemikali ndani yake, na kuifanya nyeusi." Ipo rangi moja tu asilia, na hiyo ni nyeupe. Rangi zingine zote ni upotofu kutoka kwa hiyo. Na sasa ninasema . . . Halafu basi kama ungeivunja kutoka hapo, na labda ungesema, "Vema, iligeuka kuwa asidi wakati ilipoanguka kwenye kipausha. Iligeuka kuwa asidi." Vema, basi asidi ilienda wapi? "Asidi ilirudi . . . "

Sasa, ni rangi tunayozungumzia katika hili, rangi.

111 Unasema, "Ilirudi kuwa chembechembe ndogo. Vema," wasema, "chembechembe ndogo nne mara sita ongezea tisa, hufanya chembechembe H." Kama ingetokea nne ongezea sita ongezea nane, ingetokea nini? Rangi ya waridi badala ya nyeusi. Ndipo ikarudi kutoka hapo kuwa atomu. Halafu, kutoka kwa atomu, ongeza moja ongeza B2 ongeza tatu, inafanya nne, ambayo iliiweka na molekuli H. Inamaanisha kitu gani? Ndipo unarudi kwenye nyeusi tena. Na ndipo unapoenda zaidi ya hiyo, huenda ukafikia elektroni.

112 Unaenda wapi kutoka hapo? Itakubidi kurudi. Kwa sababu ni kiumbe, ilibidi kitoke kwa Muumba. Inakubidi kukitengeneza. Hivyo basi, kilirudi kote mpaka kwa Muumba wake. Rangi hiyo iliyokuwa katika wino huo, haiwezi kurudi tena.

113 Sasa, Mungu aliona kwamba damu ya mafahali na mbuzi isingeweza kuondoa dhambi. Kamwe hakutengeneza, lakini Yeye aliumba kemikali katika Damu ya Yesu Kristo. Amina. Dhambi hiyo mara ikiungamwa kwa njia sahihi; ha—hata huweki daraja kwenye hilo shimo kubwa, unaliondolea mbali kabisa hilo shimo, na Mungu hata hajui kwamba uliwahi kutenda dhambi. Hiyo ni kweli. Alisema Yeye "aliziweka katika Bahari ya Usahaulifu," asizikumbuke tena hata kidogo dhidi yako. Basi wanaume na wanawake wanasimama katika Uwepo wa Mungu, kama wana na binti za Mungu, asili yenyewe ya Mungu wao mioyoni mwao.

114 Kanisa liko wapi leo hii, ndugu? Ni nini kilichofanyikia kanisa? Wakati, tunaweza kuona kwamba Damu ya Yesu Kristo imeondoa dhambi sana, hata Mungu hakumbuki kuwa tulitenda

dhambi. Ndipo, "Lolote mwombalo katika Jina Langu, hilo nitalitenda." Shida ni nini? Ni kwa sababu mtu fulani amekuwa akiyatia kasumba Maandiko haya kwa watu. Hili ndilo jambo pekee niwezalo kuwazia limefanywa, kwa sababu tiba ya Mungu ingali ile ile. Sasa, ni hatari kukataa chanjo ya daktari, zaidi jinsi gani Mungu!

115 Sasa mtu anapataje dawa, hata hivyo, kufanya kazi juu ya mwanadamu? Unajua kile wanakemia hufanya, au—au wanasayansi? Wanachukua ugonjwa, na kuchunguza ni kijidudu cha aina gani kilicho ndani yake, halafu wana namna fulani ya sumu, makata, na kadhalika, sumu ya kutosha kukuua, na makata ya kutosha kuizuia isikuue, nao wanaidunga kwanza ndani ya nungubandia. Wanampa huyo nungubandia ugonjwa huo ulio nao. Ndipo basi wanatia dawa ndani ya huyo nungubandia, na iwapo nungubandia atapona, basi wanakupa hiyo. Kwa hiyo hilo ni jambo kwelikweli, mwajua; kumpa nungubandia na kuona kama anaweza kuimudu, na, nungubandia asipokufa, basi wanakupa hiyo. Si wote—si watu wote walioumbwa kama nungubandia, mwajua, kwa hiyo hu—huwaua wengine na—na kusaidia yule mwingine.

116 Lakini lipo jambo moja kuhusu chanjo hii ambayo Yesu Kristo anatoa, husaidia kila mtu. Si tiba; ni uponyaji.

117 Umewasikia watu wakisema leo hii, "Mwuaji namba moja ni ugonjwa wa moyo." Na—natofautiana nao; si kuwa tofauti. Ninatofautiana tu kwa sababu ninajua kuwa ni kosa. Mwuaji namba moja ni ugonjwa wa dhambi. Kweli, si—si magonjwa yote ya moyo, ni ugonjwa wa dhambi.

118 Unajua, watu wengine husema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, ninaamini ulivuta blanketi hapo kidogo. Sasa hebu nikuulize jambo fulani. Mwanadamu hana budi kutenda dhambi; sina budi kutenda dhambi kidogo kila siku." Hiyo ni kwa sababu hujawahi kuchanjwa. Hivyo tu. Unaona? A-ha. Naam. Kamwe hukuijaribu dawa ya Mungu. Hiyo ni kweli. Kama ungefanya hivyo, basi usingefanya hilo.

119 Unasema, "Inanibidi tu kuvuta sigara. Kitu fulani hunifanya tu nivute sigara." Ijaribu chanjo wakati mmoja, na uone kama—kama inafanya kazi au la. Unasema, "Mimi—mimi siwezi kujizuia kufanya *hili*. Mimi—mimi . . . " Vema, wewe—wewe chukua tu dawa ya Mungu wakati mmoja na uone jinsi inavyokufanyia.

120 Mwanamke fulani aliniambia muda si mrefu uliopita. Nilikuwa nikimkemea kuhusu kuvaa maskini nguo hizi ndogo za aibu. Na yeye akasema, "Sasa, Ndugu Branham, hebu nikwambie, huna haki ya kusema hilo. Tunayo haki kuvaa kaptura tukitaka."

121 Nikasema, "Nadhani hiyo ni kweli. Lakini kama ulikuwa ni Mkristo, usingetaka kuzivaa." Akasema, akasema . . .

122 Ndipo yeye akasema, "Vema, sasa ngoja, Ndugu Branham." Akasema, "Unajua, hawatengenezi aina nyingine yoyote ya nguo ila tu nguo hizo za kizinifu, na kadhalika, namna hiyo."

123 Nikasema, "Wangali wanavyo vitambaa vizuri na kutengeneza cherehani. Hakuna udhuru." Hiyo ni kweli.

124 Ni kwa sababu hawataki kuchukua chanjo ya ujazo wa Roho Mtakatifu, wa mtindo wa kale, kuokolewa na Mungu, utakatifu wa mkutano wa kambi. Amina. Hiyo ni kweli.

125 Ilikuwa ni kosa kufanya mambo hayo. Bado ni kosa! Hiyo ni kweli. Lakini shida ni kwamba, kuna jambo lililotendeka. Ilikuwa kwamba—kwamba watu ambao wangetenda namna hiyo, hata walitengwa kutoka kwa jamii; sasa hawawezi kuingizwa katika jamii mpaka wafanye hilo. Na kwa hiyo, unaona, inategemea mahali moyo wako ulipo, hapo hazina zako zipo pia; ama mahali hazina yako, moyo wako upo, pia. Huna budi kukumbuka, kwamba, kama unampenda Bwana kwa moyo wako wote, utaishi safi na mtakatifu.

126 Mimi na mke wangu tulienda kwenye duka kubwa, hapa wakati fulani uliopita. Tuliona kitu cha kigeni, mwanamke aliyevalia gauni. Kilikuwa ni kitu cha kigeni katika nchi yetu. Ndipo Meda akaniambia, akasema, "Bill, ninajua kwamba, hao, baadhi ya wanawake hao huimba katika kwaya hapa chini katika makanisa." Tena akasema, "Ninawajua." Ndipo akasema, "Sasa, mbona, ni kitu gani kinachowafanya?"

127 Nikasema, "Vema, unaona, mpenzi," nikasema, "nikiwa ni mmishenari, kama nilivyo," nikasema, "sisi—sisi ni wa nchi tofauti."

Akasema, "Ati nini?"

Nikasema, "Sisi ni wa nchi tofauti, taifa tofauti."

Akasema, "Hivi sisi si Waamerika?"

128 Nikasema, "Tunaishi hapa, bali hapa si nyumbani kwetu. Sisi ni wasafiri. Tunatafuta Mji, ambao Mjenzi na Mbuni Wake ni Mungu. Nilienda huko Finland; nikaona jinsi wanavyotenda huko Finland. Nikaingia, na chini katika Ujerumani; niliona jinsi walivyo na roho ya Kijerumani. Nikateremka huko Uswisi; walikuwa na roho ya Uswisi. Nikaja Marekani; wana roho ya Kimarekani."

Akasema, "Vema, basi, vipi kutuhusu sisi?"

129 Nikasema, "Sisi tumezaliwa kutoka Juu, Mbinguni, ambapo usafi, na utakatifu, na haki, na uaminifu." Naam. Nikasema, "Hivyo basi, wale wanaokiri hilo, hawaangalii mambo ya ulimwengu huu. Bali tunasema dhahiri, kwa maisha yetu na jinsi tunavyoishi, kwamba tunaye Mungu, tunao Ufalme, tuna mahali ambako tunaelekea. Na hapa si nyumbani kwetu." Amina.

130 Jamani, ninapenda hilo! Ninaanza kujihisi kubarikiwa sana sasa hivi. Naam, bwana. Ninaamini wokovu huu wa kale, wa

Roho Mtakatifu. Loo, ndugu, dada, hufanya jambo fulani kwako. Mungu yeye yule, aliyeishi wakati mmoja, angali anaishi leo. Ninii lake lile lile, fundisho Lake lile lile la utakatifu, linaishi tu usiku wa leo sawa na lilivyowahi kuishi, kitu kile kile tu. Naam, bwana. Tazama, watu wameondokea fundisho Lake, ni hayo tu. Naam. Sasa, naam, bwana.

131 Nanii wetu namba moja . . . Ugonjwa wa moyo haufanyi, kitu hasa kinachowaua watu leo hii. Ni namba moja: ugonjwa wa dhambi. Na dhambi ni kutokuamini. Kutokuamini nini? Biblia. Hiyo ni kweli. Naam, ndio namba moja: ugonjwa wa dhambi, unaowaua watu leo hii, zote mbili kiroho na . . . Na hiyo itawafanya kuwaua kimwili, bila shaka, maana tayari wanaweza kuthibitisha kwa watu wanaoshikilia kinyongo, na wanawake wanaozozana na kuwa na hamaki, na kupigana na kubishana, wanakufa. Itasababisha kansa, fangasi, kila kitu kingine kitaingia, vidonda.

132 Unaona, uliumbwa kuwa na furaha na huru. Uliumbwa kuishi kama watoto mbele za Baba yenu, na—na kujua kwamba Yeye hufanya kila siku, kila kitu kufanya kazi vizuri kwako kila siku. Naam, bwana.

133 Watu wanaogopa tu huku Kuzaliwa kupya. Ni hayo tu. Wanaogopa kukujia, kwa sababu kutawanyoosha kabisa. Kutakufanya uache kucheza kamari, uache kucheza hizi mashine za bahati nasibu. Kutakufanya uache kukaa nyumbani Jumatano usiku, mbali na mkutano wa maombi, kutazama *Tunampenda Sucy* na vitu hivyo vyote vya wazimu Hollywood ilivyo navyo, na mizaha hiyo michafu inayotolewa huko. Na kutafanya—kutakufanya uache nywele zako zikue, ndefu. Kutakufanya kutenda kama mama wa heshima. Kutamfanya mwanaume kuacha kuvuta sigara, huku wakiwa kanisani kama mashemasi. Kutawafanya watu waache kusema uongo, kuiba. Kutakufanyia jambo fulani. Kutakusafisha kabisa na kukupa wokovu hata hakuna chochote ulimwenguni kiwezacho kuuelezea mbali hata utoke kwako, maana unajua ulikuwa hapo wakati kulipotendeka. Naam, bwana.

134 Sasa, kama nilivyosema muda mfupi uliopita, wakati Mungu . . . Wakati mtu akipata dawa, kitu wafanyacho, wanatafuta tiba hii. Ndipo wanagundua ugonjwa huu, halafu wanauingiza ndani ya nungubandia kwa sindano na kuona kama nungubandia atapona huo.

135 Sasa, wakati Mungu alipokuwa anaenda kushusha chanjo hii ambayo ninazungumzia usiku wa leo, zeri hii ya Gileadi, Yeye hakumchukua nungubandia. Alikuja Mwenyewe. Amina. Njia pekee Yeye aliweza kufanya, ni kuja katika umbo la Mwana Wake, na alifanyika mwili na akakaa miongoni mwetu, ili kuondoa mwiba wa kifo. Yeye alikuja ili kufa. Njia ya pekee Yeye angaliweza kufa . . . Asingeweza kufa kama roho, kama mwanadamu. Kwa hiyo Yeye aliumbiwa mwili uitwao

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, na Mungu akakaa ndani ya mwili huu, akijifanya Mwenyewe Imanueli duniani, ili kuondoa dhambi ya mwanadamu. Hiyo ilikuwa ndiyo kemia iliyokuwa katika Damu hiyo.

136 Mtu fulani alisema, “Yeye alikuwa ni Myahudi.” Yeye hakuwa Myahudi. Baadhi yao walisema, “Yeye alikuwa ni Mtaifa.” Hakuwa Mtaifa.

137 Yeye alikuwa si chochote pungufu ya Mungu. Biblia ilisema kwamba, “Tumeokolewa kwa Damu ya Mungu.” Damu hutokana na jinsia ya kiume. Tunajua hilo. Himoglobini hutoka kwa mume; mke ni yai tu. Hiyo ni kweli.

138 Kama nilivyosema pale, kama wakati wa kuchipua. Maskini hawa mama ndege wanajenga viota hapa nje, na kutaga mayai. Baadhi yao watataga mayai yaliyojaa kiota ambayo kamwe hayataanguliwa, pia. Kwa nini? A—angeweza kutaga mayai kujaza kiota, na angeweza kuyakalia na awe tu mwaminifu. Angeweza kuyageuza mayai hayo kila siku, na kukaa hapo mbali na chakula, mpaka awe mnyonge sana hata asingeweza kuruka kutoka kwenye kiota. Haijalishi ni kiasi gani anayabembeleza, na ni kiasi gani anayapapasapapasa, na jinsi alivyo mwaminifu kwayo, kamwe hayataanguliwa. Kwa nini? Hajawahi kukutana na mwenzi wake, nayo hayajarutubishwa, hivyo basi yatakaa tu hapo na kuoza.

139 Hiyo ndiyo shida na mikutano yetu mingi. Hiyo ndiyo shida ya mkutano wetu wa kambi, mingi ya hiyo leo hii, na mikutano yetu. Tunapata nini? Kundi la wanyama marafiki na wahubiri dhaifu wanaopaswa . . . Mbona, ni aibu. Na kuingia humo ndani kwa sababu ana hadhi kubwa kidogo, ama elimu kidogo, kuwainua juu ya kitu fulani. Ningeninii, jamani, kitu pekee tunachohitaji leo hii ni . . . Tunacho kiota kilichojaa mayai yaliyooza.

140 Tunachohitaji ni wakati mzuri wa kale wa kukisafisha kiota, kote kuanzia hapo, kutakakokisukuma kutoka hapo, mpaka tupate wanaume na wanawake waliojazwa na Roho Mtakatifu; ambao wamekuwa na Mwenzi wao, Yesu Kristo, na wamejazwa na Roho ambaye Yeye alibatizwa naye. Hiyo ni kweli. Ndipo tuna Uzima kwenye kambi. Naam, bwana. Dawa, wanaogopa Hiyo.

141 Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, wakati Yeye alipozaliwa, baadhi yao walisema, “Vema, sasa, Yeye alikuwa, Yeye—Yeye alikuwa ni yai la Mariamu.” Hakuwa. Kama Mariamu ilibidi ashushe yai hilo kupitia kwenye tyubu hadi kwenye tumbo la uzazi, ilibidi kuwe na msisimko, kwa hiyo unaona kile unachomweka Mungu kufanya? Yeye hakuwa hata, si sehemu yake hata.

142 Mungu, Muumba, alimtia uvuli bikira Mariamu, na kuumba seli ndani ya tumbo lake la uzazi, akamzaa Mwanaume aliyekuwa Imanueli, Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili,

miongoni mwetu, bila usaidizi kutoka kwa mtu yeyote. Yeye ndiye Muumba aliyemwumba mtu wa kwanza. Amina. Loo, jamani! Huyo hapo. Hapo Yeye amesimama. Naam, bwana. Ndipo basi Yeye alifanya hilo ili Yeye aweze kuchukua chanjo.

143 Mwanasayansi yeyote mzuri halisi, daktari mzuri anayegundua ugonjwa, baadhi yao wataenda kwenye kambi ya gereza na kuchukua mtu fulani ili kuijaribu, ambaye anaenda kuwa na kifungo cha maisha gerezani. Akiponea chanjo hiyo, mbona, basi sumu hiyo isipomwua, anaweza kuwa huru ikiwa yuko tayari kuchukua chanjo hiyo. Wafungwa hungojea hiyo. Loo, huyo ni daktari anayeogopa dawa yake.

144 Bali, mnajua, Mungu hakuogopa dawa Yake Mwenyewe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . katika hori, mtu aliyesimama kwenye kingo za Yordani. Wakati chanjo ilipoanguka pale chini, aliiona kama hua akishuka chini toka Mbinguni, na Yeye alitiwa chanjo. Ndipo Sauti ikasema, "Huyu ni mwana Wangu mpendwa ninayependezwa kukaa ndani yake." Amina. Mungu ndani ya mwanadamu. Hiyo ndiyo chanjo. Mungu ndani ya mwanadamu. Ulimwengu ulimtazama Yeye. Kila jaribu, Yeye alishinda. Wakati walipomtemea mate usoni Mwake, wakang'oa ndevu na kumtemea mate, Hiyo ilihimili majaribu. Katika majira ya majaribu, ilishinda majaribu. Ilishikilia! Chanjo ambayo Yeye alipokea pale Yordani, ilishikilia. Ilishikilia katika wakati wa umaarufu.

145 Kuna shida gani na mengi ya—ya makanisa leo, Mungu atayabariki, yanaanza . . . Na hiyo ndiyo inayoumiza watu wetu Wapentekoste. Wao, wao wanapaswa kurudi nyuma kama babu zetu walivyokuwa, wakiwa na kikaango cha bati au tari, chini pembeni mahali fulani, wakipiga tari; kuliko vile ingekuwa kulala katika vyumba hivi vikubwa vya kuhifadhia maiti ambavyo tunajenga leo hii, tukijaribu kujifananisha na watu wengine. Tunachohitaji ni umwakikaji mzuri wa Roho Mtakatifu wa mtindo wa kale, ambao utakusafisha, pamoja na nyinyi wachungaji wa kanisa la Pentekoste. Hiyo ni kweli.

146 Sasa, jambo lilikuwa, kwamba wakati Roho Mtakatifu aliposhuka juu ya Yesu, kwenye siku ya kubatizwa Kwake, Yeye alitiwa chanjo. Tumemwona Yeye katika saa ya majaribu. Wakati ibilisi alipojaribu kumpatia Yeye falme zote za ulimwenguni, Yeye alifanya nini? Alidumu moja kwa moja na Neno. Amina.

147 Kinachonishangaza leo hii, kwamba ndugu wengi nje hudumani tangu uamsho huu wa siku ya mwisho . . . Ni kwa nini, unapopata vijisenti vichache au nguo za kubadilisha, wewe ni mkubwa kupita kiasi kuenda mahali fulani, pia, loo, kitu kingine, na inakubidi kuwa na kitu kikubwa kuliko yule mwingine? Imekuwa ni mashindano ya kawaida ya cheo. Ni aibu. Mungu anataka mtu ambaye atajinyenyekeza, na kufikia chini mahali fulani, mtu ambaye Yeye anaweza kumzungumzia.

Lakini imekuwa ni mashindano makubwa ya cheo, kila mtu anajaribu kupata kitu fulani kikubwa kushinda huyo jamaa mwingine. Ni . . . Na, unaona, hawawezi kustahimili hiyo hadhi ya jaribu la Shetani.

148 Bali Bwana wetu aliyashinda majaribu. Chanjo ilishikilia. Wakati ulipowadia, kulikuwa na majadiliano juu ya Maandiko, Yeye alidumu moja kwa moja na Neno. Shetani alisema, "Imeandikwa."

Yeye akasema, "Pia imeandikwa." Loo, ni . . . Utukufu! Mungu ndani ya mwanadamu, unaona.

149 Yeye alikuwa na kitu gani? Alikuwa na kitu fulani pamoja Naye kuunga mkono kila neno ambalo Yeye alisema. Alisema, "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Bali ikiwa hamwezi kuniamini Mimi, amininі—aminini kazi ambazo Yeye anafanya kupitia Mimi." Loo, jamani! Haya basi.

150 Tunachohitaji ni wanaume na wanawake kama hao, leo hii, ambao wanaweza kufunga kinywa cha ulimwengu, kwa ishara za Roho Mtakatifu. Tunahitaji mkutano wa kambi namna hiyo. Tunahitaji kupinduliwa juu chini, kutikiswa, ulimwengu mwingi na vitu kutoka kanisani, ambavyo vimeingia ndani katika siku hizi za mwisho. Pesa zinasambaa kote nchini, na vitu vikubwa, ambavyo vimeweka nia za watu juu ya vitu vikubwa badala ya juu ya Mungu. Kupatana, kupatana juu ya Maandiko! Ndugu yeyote aliyeanza katika njia hiyo, bali wanakuwa maarufu katika dhehebu fulani, kupatana juu ya kile alichoamini.

151 Damu hiyo haitiririki ndani ya mtu halisi, aliyezaliwa na Roho Mtakatifu. Pepo wote wa kuzimuni hawawezi kumwondoa kwenye Neno hilo. Atasimama juu ya Hilo bila kujali chochote. Amina. Paulo alisema, "Hakuna chochote kilichopo au kitakachokuwepo, kiwezacho kuja, au chochote, kiwezacho kututenganisha na upendo wa Mungu." Huko kuzaliwa halisi kwa kweli na Roho Mtakatifu huja ndani ya mtu, yeye ni mwana wa Mungu. Hakuna shimo kati yake na Mungu. Yeye ni mwana Wake katika Uwepo Wake. Amina. Ninapenda hilo. Ninajua hilo ni kweli. Vema.

152 Tunaona kwamba katika saa ya majaribu, kwa mambo ya ulimwengu, chanjo ilishikilia. Katika wakati wa kuitwa mtakatifu anayejibingirisha au—au kudhihakiwa, kuwekwa kitambaa usoni Mwake, macho Yake, na kumpiga Yeye kichwani kwa fimbo, kasema, "Sasa, ikiwa Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga Wewe." Hao askari wa Kirumi, walimwona Yeye akitambua mawazo ya watu. Kujitokeza na . . .

153 Kama Yeye alikuwa amesimama hapa usiku wa leo, Yeye angeangalia kote na kumwambia mwanamke huyo kilichokuwa shida yake, na kile kilichokuwa *hiki* na *kile*. Hivyo ndivyo alivyofanya hilo. Hivyo ndivyo Yeye angali anavyofanya, maana

Yeye habadiliki. Amina. Hivi hamna furaha? Huyo ni Mungu aishiye. Kwamba mtu angeweza kuanguka kutoka kwenye paa, na uhai utoke ndani yake; na mtu aliyesimama hapo akiwa na Mungu ndani yake, angeweza kujilaza mwenyewe juu ya mtu huyo, naye akaishi tena. Mungu yuyo huyo anaishi usiku wa leo. Amina. Yeye ni Mungu asiyebadilika. Kanisa linahitaji chanjo. Hiyo ni kweli.

154 Kama David duPlessis alivyosema wakati mmoja, Mungu hana wajukuu. Hiyo ni kweli. Mahali ambapo ndugu zetu Wapentekoste wanafikia, watoto wao wanaingia kanisani na kusema tu, "Vema, sisi ni Wapentekoste maana baba alikuwa." Kama baba alikuwa ni Mpentekoste, na akapata ubatizo wa Roho Mtakatifu, itakubidi kumpokea Huyo sawa na baba alivyompokea. Yeye hana wajukuu. Yeye anao wana na binti pekee, sio wajukuu wa kiume na wajukuu wa kike; wa—wana tu na binti. Ni kweli.

155 Kwa hiyo inakubidi kufanya jambo lile lile walilofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Inakubidi kuwa na tukio lile lile. Inakubidi kuwa na kitu kile kile walichokuwa nacho. Mungu kamwe habadilishi utaratibu Wake. Yeye kamwe habadilishi njia Zake. Yeye hufanya tu jambo lile lile wakati wote. Jinsi anavyoweka mpango Wake, lazima ufuate huo kila wakati. Inabidi iwe ni jambo lile lile. Na kama utafanya jambo lile lile, matokeo yale yale yatakuja. Amina. Hiyo ni kweli.

156 Sasa tunaona, ilistahimili katika wakati wa majaribu. Ilistahimili wakati kila kitu kilikuwa kinaenda vibaya. Ilishikilia wakati rafiki Zake wote walipomwacha. Yeye angali alishikilia, chanjo ilishikilia. Ndipo ibilisi akawazia, "Nimempata sasa." Alianza kuelekea Kalvari, Damu ikibubujika kutoka mwilini Mwake. Amejizungushia vazi Lake, kurashia kumoja kukubwa kwa Damu. Ibilisi lazima alisema, "Nimempata sasa. Huyo hawezi kuwa ni Mungu. La, la. Huyo hawezi kuwa ni Yeye, kama Yeye angeweza kuwaruhusu askari kumtemea mate usoni Mwake, kama Yeye angewaacha wang'oe makozi yaliyojaa ndevu kutoka usoni Mwake, kama Yeye angewaacha wampe changamoto kuona ono na Yeye hakufanya hivyo. Na sasa hapa Yeye anapanda juu ya kilima, akibeba huo msalaba, nitampata Huyo katika dakika chache."

157 Huyo nyuki wa mauti akashuka, na akizunguka, ili kumwuma Yeye. Unajua, kama nyuki yeyote, anao mwiba ndani yake. Bali, unajua, Mungu alikuwa ametayarisha mwili wakati huo, ulikuwa ni mwili wa Mungu. Wakati mwiba huo ulipotiwa ndani ya huyo Mwana wa Mungu kwa wakati mmoja, ndani ya Imanueli; wakati alipojivuta kujitoa mwenyewe, alikuwa hana mwiba wowote uliosalia. Yeye aliondoa mwiba moja kwa moja kutoka kwa mauti. Si ajabu Paulo angeweza kusema, "Mauti, wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini

shukrani kwa Mungu, Yule ambaye hutupatia ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo."

158 Angeweza kumdunga Eliya, na kufa, angeweza kumdunga Eliya na abaki na mwiba wake. Bali, mwajua, nyuki aki—nyuki akiwahi kumdunga mtu kwa kilindi vya kutosha, hawezi kudunga tena, yeye huvuta na kutoa mwiba wake. Kwa hiyo hakukuwa na mwili wowote wa mwanadamu alioweza kuutia ndani yake. Loo, jamani! Hakuna mtu aliyeweza kuutia ndani yake. Bali alipoutia ndani ya Imanueli wakati huo, alipoteza mwiba wake. Shukrani kwa Mungu! Naam, bwana, alishindwa kwa huyo. Naam, bwana.

159 Waligundua kwamba dawa hiyo ilihimili. Walisema, "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani." Kuhani mkuu, mwenye cheo kikubwa kanisani, alisema, "Tuambie waziwazi sasa. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka chini kutoka msalabani na ujiokoe Mwenyewe," na kadhalika. "Hebu tuone kama Wewe ni Mwana wa Mungu." Kamwe hakufungua kinywa Chake na kusema neno.

160 Sasa tunaona kwamba Yeye alikufa. Alikufa kwelikweli. Alikufa mpaka jua na mwezi zikasema Yeye alikufa. Maumbile yote yalisema Yeye alikufa. Nchi ikatetemeka, ilikuwa na baridi ya wasiwasi ikipita juu yake. Basi walipomwona Mungu mwenyewe ambaye aliumba nchi, alikuwa amening'inia juu ya nchi, na Damu ya Imanueli ikidondoka juu ya nchi. Si ajabu Yeye alikufa. Alikufa mpaka kila kitu kikasema kuwa Yeye alikufa.

161 Na kisha tunaenda kuona, kabla Yeye hajafa, alisema, "Liharibuni hekalu hili, nami nitalisimamisha tena kwenye siku ya tatu. Hamtaweza kulishikilia chini. Liharibuni, nami nitalisimamisha tena kwenye siku ya tatu."

162 Wakaweka ulinzi kote, kuona kama chanjo hiyo ilikuwa inaenda kushikilia. Waliona ilishikilia kupitia majaribu ya dhambi. Ilishikilia kupitia umaskini. Ilishikilia kupitia utajiri. Ilishikilia kupitia kila namna ya majaribu. Ingali ilishikilia. Bali sasa iko katika mauti, inaenda kufanya nini sasa?

163 Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, loo, jamani, kabla tu ya hilo jua kuchomoza, chanjo hiyo ilishikilia. Na, wakati iliposhikilia, kifo kikavunja vizuizi vyake, kaburi likafunguka, ndipo Yeye akafufuka tena kwenye siku ya tatu na kupaa Juu. Inaonyesha kwamba chanjo hiyo ndiyo chanjo ya Uzima wa Milele. Huwezi kuiangamiza. Hata tumbo la kuzimu haliwezi kuishikilia. Kaburi haliwezi kuishikilia. Kifo hakiwezi kuishikilia. Hakuna chochote kinachoweza kuishikilia. Itafufuka tena.

164 Yesu Kristo alisema, "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, nami nitawafufua tena kwenye siku ya mwisho." Haleluya! Mwanaume au mwanamke ambaye ametiwa chanjo na Hii, hawezi kubakia kaburini. Hakuna kaburi linaloweza

kumshikilia mwenye haki. Hakuna kuzimu kunakoweza kuishikilia; hakuna kaburi, hakuna chochote kingine. Yesu Kristo aliahidi kulisimamisha tena kwenye Siku hiyo. Amina. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya hiyo, hiyo chanjo. Unajua, kwenye asubuhi ya Pasaka ilithibitisha.

165 Je! unajua ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni kitu kikuu sana, hata watu mia moja na ishirini walitaka kupata chanjo. Sasa, kama Yeye anaweza kudumisha kupitia majaribu, kulikuwa na watu mia moja na ishirini waliomjua Yeye vizuri sana, walihitaji hiyo chanjo. Kwa hiyo moja kwa moja basi ilimbidi Yeye kwenda kwenye maabara na kutayarisha dawa ya chanjo, kwa hiyo Yeye alisema, "Nyinyi nendeni huko juu kwenye mji wa Yerusalemu mpaka niipate, kanuni yote iwekwe sawasawa. Ninaenda kuituma Hiyo chini kwenu." Kwa hiyo walipanda juu kungojea.

166 Jinsi kanisa la Kikristo linavyopaswa kuendeshwa, ni chanjo ya aina gani lingehitaji? Nini, nini ingekuwa ndiyo chanjo? Wangefanyaje? Ni nini kingetukia? Je! wote wanapaswa kuenda kwenye seminari na wajifunze kuwa na Ph.D. na LL.D.? Je! kasisi fulani anapaswa kuja barabarani akiwa na mkate mwemmbamba mikononi mwake, na kutoa ulimi na kula ushirika, na hayo yatosha?

167 "Bali kulikuja sauti kutoka Mbinguni," chanjo ilikuwa inakuja, "kama upepo mkuu unaovuma, na Hiyo ikajaza nyumba yote mahali walipokuwa wameketi. Ndimi zilizogawanyika zikawakalia juu yao, kama Moto. Na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."

168 Hivi mliwahi kuona hekalu la kale, picha yake? Kulikuwa na mlango mdogo wa pembeni wa kutokea, ukaenda kupitia vipandio, kuenda katika chumba cha juu. Walifunga milango na kuingia ndani, kwa sababu waliogopa.

169 Bali ninawaambieni, walipotiwa chanjo kama ndama aliyetiwa chapa mpya, wasingeweza kumtuliza. La, bwana. Kutoka katika chumba hicho alikuja, akatoka akaingia mitaani. Alitiwa chanjo. Kifo, kuzimu, mateso, kuchekwa, kudhihakiwa, hakukuleta tofauti yoyote kwake, alikuwa ametiwa chanjo. Amina. Loo, jamani!

170 Msikilize Petro akisimama kule. Walianza kuuliza, "Hivi kuna zeri zaidi katika Gileadi? Je! kuna zeri zaidi katika Gileadi? Je! hakuna tabibu huko?" Loo, naam, tuna zeri chungu nzima katika Gileadi. Tuna matabibu wengi.

171 Katika siku hiyo, Daktari Simoni Petro, alikuwa ndiye tabibu. Alisema, "Ninaenda kuwaandikia dawa. Ninaenda kuwaambieni. Na hili ni agizo la Milele, kwa sababu litakuwa ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio

mbali. Kusema kweli, ni kwa ajili ya kila mtu ambaye atamwitia, Bwana Mungu wako atamwita, 'Nitampa hilo.'"

172 Kasema, "Tunaweza kufanya nini ili kuweza kutiwa chanjo?" Hapo ndipo alipo. "Tunaweza kufanya nini ili tuweze kutiwa chanjo?"

173 Akasema, "Nitaandika dawa." Akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa agizo hili ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Loo, jamani!

174 Unajua nini? Daktari akipata suluhisho la ugonjwa; naye anaandika agizo, ndipo mwuza dawa fulani mbabaishaji analichukua na kuanza kuongeza kidogo cha *hiki* na kutoa kidogo cha *hiki* kutoka kwa hilo, ama atamwua mgonjwa au— au kufanya jambo fulani kwake. Agizo hilo hata halina dawa za kutosha ndani yake kufaulisha chochote. Isipofanya, ni dhaifu sana hata hutamsaidia mgonjwa.

175 Na hiyo ndiyo shida na wengi wa hawa wauza dawa wa seminari leo hii. Wanachukua agizo, na kuongezea kitu fulani badala ya Hilo, na una lundo la vyumba vya kuhifadhia maiti vinavyokufa.

176 Agizo hili lingali linabaki vile vile. Wakati Wasamaria walipopokea Hilo, walipewa chanjo, walikuwa na kitu kile kile. Wakati Mataifa walipopokea Hilo, walipata agizo lilo hilo. Paulo alikutana na kundi katika Matendo 19, ambao walikuwa na sehemu ya agizo, si Hilo lote, akasema, "Hilo halitafanya kazi. Mnaenda kuua kitu chote." Kwa hiyo akaliandika, kwa ajili yao, akawaambia jinsi ya kulipata. Walilipata vivyo hivyo.

177 Na hiyo ndiyo shida leo hii. Kuna zeri chungu nzima katika Gileadi, na tuna matabibu wengi, ila watu wanaogopa dawa. Utukufu! Sifa kwa Mungu. Je! hakuna zeri katika Gileadi? Je! hakuna nguvu za Roho Mtakatifu? Sasa zipo?

178 Chanjo *hii* hufanya kazi juu ya wote, unaona. Ilifanya kwa Wayahudi. Ilifanya kwa Wasamaria. Ilifanya kwa Mataifa. Hufanya kwa kila mtu vivyo hivyo.

179 Mimi ni mmishenari. Ninaenda katika nchi ambamo watu huko ambao hata hawajui ni upi mkono wa kulia na wa kushoto, nao wanasimama hapo. Unajua wanalofanya wakimpokea Roho Mtakatifu? Jambo lile lile mnalofanya, jambo lile lile.

180 Loo, ni kitu gani? "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwao walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Agizo lili hili hutimiza jambo lile lile.

181 Nalo kanisa litafanya jambo lile lile lililofanya huko mwanzo. Kweli kabisa. Yesu ndiye mzabibu. Sisi ni matawi, na kwa kutiwa chanjo na ule Uhai uliokuwa katika mzabibu.

Kanisa lililotoka, likatiwa chanjo, waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake.

182 Sasa tunavyo vibadala fulani. Tunayo matunda fulani yaliyopandikizwa. Hu—huishi kutokana na uhai wa mti, bali halitazaa matunda. Hiyo ni kweli.

183 Nilikuwa nimesimama na rafiki yangu, John Sharrit, kule Phoenix, hapa si muda mrefu uliopita. Alikuwa na mti huko, mchungwa, ambao ulikuwa na yapata matunda matano au sita mbalimbali juu yake.

Nikasema, "Sijawahi kuona kitu kama hicho."

Akasema, "Imepandikizwa."

Nikasema, "Ni mti wa aina gani?"

Akasema, "Mchungwa."

184 Nikasema, "Vema, kuna limau, na kuna ndimu, na kuna chenza, na makangaja, na—na balungi, aina nyingi mbalimbali." Nikasema, "Na yote yamekuzwa kutokana na mti huo mmoja?"

Akasema, "Naam, yote ni matunda jamii ya chungwa."

185 Nikasema, "Vema, sasa, hicho ni kitu cha ajabu." Nikasema, "Sasa, mwaka huu, baada ya tunda hilo lote kutoweka, mwaka ujao utazaa chungwa?"

186 Akasema, "Loo, la. Ha-ha. La." Kasema, "Utazaa aina liliyo tawi hilo."

187 Ndipo nikasema, "Basi mti huo uligeuka kutoka, unamaanisha, kutoka kwa m—chungwa kuwa kile . . . "

188 Akasema, "La, la, la. Ukiwahi kutoa tawi jingine, litazaa chungwa."

Nikasema, "Naona." Amina.

189 Ndugu, tunavyo vitu kama madhehebu ya kanisa vilivyopandikizwa kwenye Hili, na vinaishi kutokana na Hili, vikijiita vyenyewe Wakristo. Lakini ikiwa Uhai halisi wa mti huo utawahi kuzaa tawi jingine lake mwenyewe, litakuwa ni Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake, kwani Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Kile ulimwengu na hazina zake, nao hawajui chochote juu yake. Watu wanaisoma Biblia hii, kama ukisoma Hii kutokana na mtazamo wa kidhehebu, hutapata mengi kutoka kwa Hiyo. Bali ikiwa utaangalia tu kile Hiyo isemacho, basi tii kile agizo lisemacho. Soma Hiyo, itii Hiyo, itafanya mtu tofauti.

190 Ndiyo kwanza nitoke India, hapa si muda mrefu uliopita. Nilimsikia mwanamke hapa, alikuwa amelemewa na umaskini, mtoto wake alikuwa ameenda India kuwa daktari. Naye alifika kule na akaacha kazi yake ya udaktari, na kuingia katika nyingine, ninaamini alikuwa ni mhandisi umeme, au kitu fulani. Ndipo mwanamke huyu akalemewa na umaskini. Kabisa hakuwa na chochote, na kwa hiyo watoa msaada walikuwa

wanajaribu kuja kumshughulikia. Na kwa hiyo walichukua jambo hilo, na wakati walipofanya uchunguzi, waligundua kwamba mama huyo alikuwa na mmoja wa kumsaidia, na huyo alikuwa ni mwanaye ambaye alikuwa ni mtu tajiri sana kule India. Ndipo kasema, "Vema, kwa nini mtoto wako hakusaidii?"

191 Kasema, "Loo, nisingeweza tu kumwomba." Kasema, "Mimi ni mama yake," kasema, "Afadhali tu nichukue msaada kuliko kumwomba mtoto wangu."

Kasema, "Hivi kamwe husikii kutoka kwake?"

192 Kasema, "Loo, mimi husikia kutoka kwake angalau mara moja ama mara mbili kwa mwezi." Kasema, "Yeye huniandikia baadhi ya barua za kupendeza sana ulizowahi kusoma."

193 Kasema, "Vema, inaonekana kana kwamba kama alimpenda mama yake vya kutosha, na alikuwa na pesa nyingi, angekuwa anajaribu kumtunza, badala ya yeye kulazimika kwenda kwa wenye kutoa msaada."

194 Kasema, "Vema, labda kama alijua nilikuwa hivi," kasema, "angeweza, angeweza kunitunza mimi. Lakini," kasema, "unajua, hajui, na mimi—mimi hujionea tu aibu kumwambia mwanangu, namna hiyo."

Ndipo kasema, "Na yeye bado hukuandikia barua za kupendeza?"

195 Kasema, "Loo, baadhi ya barua za kupendeza kuliko zote!" Tena kasema, "Yeye hunitumia picha za kupendeza kuliko zote ulizowahi kuona."

Kasema, "Picha nzuri kuliko zote? Basi hebu tuone baadhi ya hizo."

196 Akapitia kwenye Biblia yake, na akazitoa. Unajua zilikuwa nini? Hati za benki za kuidhinisha malipo. India hutia picha kwenye hati zao za benki za kuidhinisha malipo, unaona, picha za kupendeza. Alikuwa na maelfu ya dola, zikibadilishwa kutoka kwa pesa za India kuwa pesa za Marekani. Ilikuwa ni kitu gani? Katika shubaka la Biblia yake, alikuwa na hazina alizodhania zilikuwa ni "picha tu," bali, akaja kugundua, ilikuwa thamani halisi kwake.

197 Pia, ndugu, unapojaribu kusoma kuhusu moto uliochorwa wa Pentekoste, na mtu fulani anajaribu kukuambia kwamba Roho Mtakatifu si yeye yule leo kama alivyokuwa wakati ule, mtu fulani anajaribu kukuambia siku za miujiza zimepita, kwamba Yesu Kristo siye yeye yule jana, leo, na hata milele, wanavyojaribu kukuambia, usiamini hilo. Hizo si picha. Mungu Mwenyezi alikutumia ujumbe huo, hiyo ni kweli, "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Mungu angali ni Mungu. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

198 Yeye yupo papa hapa, usiku wa leo, kuwaokoa waliopotea, kuwaponya wagonjwa, kujaza na Roho Mtakatifu, wale wanaotaka kujazwa. Mnaamini hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana. Kama unaamini hilo, basi, unaona, hizo ni ahadi za Mungu katika Neno hili hapa, unaweza kuingia moja kwa moja humo ndani na upate kila ahadi. Ahadi ni kwa ajili yako. Petro alisema, "Ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwao walio mbali." Usiogope kupeleka hiyo kwa ajili ya malipo. Hiyo ni hati ya benki ya kuidhinisha malipo ya Mbinguni. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo yeye yule jana na milele!

199 Vipi kama Yeye alisimama hapa usiku wa leo na kumwona mwanamke yule amelala pale mgonjwa? Anaonekana kama ni mgonjwa sana, amelemaa, labda amepooza ama kitu fulani. Wanawake wawili . . . Mwanamke, na mwanaume mweusi na mwanamke mweusi, wakijaribu kushughulika na mtoto mchanga, unafikiri Yeye angefanya nini kama Yeye alisimama akiwaangalia hao wagonjwa wawili hapo, kama mponyaji? Je! unafikiri Yeye anaweza kuwaponya? Amefanya hivyo tayari, unaona. Wakati alipokufa Kalvari, Yeye alifanya hivyo. Je! mnaamini hilo, enyi wagonjwa? Mnaamini hilo ni kweli? Wewe hapo na maskini mama mweusi, hapo pamoja na mtoto mchanga, je! unaamini kwamba Yesu Kristo, wakati Yeye alipokufa Kalvari, Yeye alinunua uponyaji wa mtoto wako?

200 Wewe kwenye kitanda cha kubebwa hapo, kama wewe ni . . . Unaonekana mgonjwa sana. Umepooza, chochote kile, hivi unaamini Yesu Kristo alikufa Kalvari, kukuokoa na ugonjwa wako? Je! unaamini hilo? Je! unaamini kwamba yale niliyosema usiku wa leo, kwamba ni kweli? Je! unaamini kwamba agizo hilo ni kweli? Unaamini?

201 Kama Yeye alisimama hapa usiku wa leo, na wewe ulimwuliza, "Hivi Wewe utamponya mtoto wangu?" Unajua kile Yeye angesema? "Nimefanya hilo tayari." Unaona, unaliamini tu. Unaona? Kama ungesema, "Bwana, nimelemaa, siwezi kutembea," ama chochote kilicho. "Si—siwezi kutembea. Ni—ninakufa," au kitu fulani, "Hivi Wewe utaniokoa?" Yeye angesema, "Nimefanya hivyo tayari." Unaona?

202 Sasa ungejuaje ilikuwa ni sauti Yake? Kwa sababu Yeye angefanya jambo kama alivyofanya wakati ule. Huenda akaweza kukuambia jambo fulani kukuhusu mwenyewe, akwambie kile ulichokuwa, ama kilicho shida yako, ama kitu fulani namna hiyo, kama Yeye alivyofanya katika wakati wa Biblia. Hiyo ingeonyesha Yeye alikuwa ni yule yule. Bali kwa uponyaji, ingekubidi kuukubali mwenyewe. "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Je! unaamini hilo?

203 Je! unaamini Yeye angeweza kuniambia usiku wa leo kilicho shida yako, ama jambo fulani kukuhusu wewe uliyelala hapo? Je! ungelikubali na kuniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Utaamini?

204 Vipi kukuhusu wewe, mama huyo hapo karibu naye, mkono wako ukiwa juu ya mtoto wako mchanga, je! unaamini hilo?. . .?. . .

205 Ni wangapi wataamini hilo? [Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."—Mh.]

206 Sasa, Baba wa Mbinguni, huyu ni mtumishi Wako. Nimeninii tu . . . Ninawajibikia tu kuhubiri Neno Lako. Sasa, ninajua hili si la kawaida, ila ninaomba kwamba Wewe utalijalia usiku wa leo, kwamba watu wataweza kujua kwamba—kwamba hii ni Kweli.

207 Vema, angalia huku. Mtoto wako mchanga ana namna fulani ya ugonjwa wa mfupa. Hiyo ni kweli. Ana uvimbe mkubwa mguuni. Hiyo ni kweli? Weka mkono wako juu yake, rudia na useme, "Bwana Yesu, mponye mtoto wangu mchanga, nitakutumikia Wewe maisha yangu yote." Kama hujawahi kuchukua chanjo hii, amini Hiyo kwa moyo wako wote. Na uweke uzi kuzunguka mguu wa mtoto huyo, usiku wa leo, na uupime. Halafu basi urudishe uzi huo kesho, mahali ulipoukatia, kiasi gani ulipunguka kati ya sasa na kesho usiku. Je! utafanya hivyo?

208 Wewe uliyelala hapo, unayefuata, je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Sijawahi kukuona, maishani mwangu. Lakini umelala hapo, umetiwa uvuli wa mauti. Kuna kivuli cheusi juu ya mwanamke huyo. Anaugua, akifa kwa kansa. Hiyo ni kweli kabisa. Na wewe unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima? Unaweza kuamini hilo? Basi kwa nini ulale hapo mpaka ufe? Daktari hawezi kuponya huo. Amka, katika Jina la Yesu Kristo, na uchukue kitanda chako na uende nyumbani.

209 [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Je! unaamini? Wote wanaotaka kuamini na kukubali uponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu na mumshukuru Mungu.

Mshike mkono, ndugu yangu.

210 Hebu tuseme, "Bwana asifiwe," kila mtu. Je! mnamwamini? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Inueni mikono yenu sasa kwa Mungu, na mumsifu Yeye. [Kusanyiko linashangilia.] Je! mnaamini? [Kusanyiko linashangilia.] Hivi hakuna zeri katika Gileadi? Nguvu za Mungu zinaweza kufanya hilo!

211 Hebu tusimame kwa miguu yetu, kila mtu sasa, tukiwa na imani kuamini hilo. Simama kwa miguu yako, kila mtu, na ukubali ukombozi, katika Jina la Bwana. Amina. [Kusanyiko linaendelea kushangilia—Mh.]

Kwa Nini? SWA63-0626
(Why?)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, tarehe 26 Juni, 1963, kwenye Uwanja wa Kambi wa Associated Brotherhood Of Christians kule Hot Springs, Arkansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org